# Nipashe

Jumanne Aprili 30, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579905

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**MITANDAO YAPONZA DIWANI**

DIWANI wa Kata ya Ngokolo Manispaa ya Shinyanga, Emmanuel Ntobi, amefukuzwa kwenye Baraza la Madiwani kutokana na...

UKURASA 3



**VIPAUMBELE ELIMU**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imewasilisha bungeni bajeti yake ya zaidi Sh. trilioni 1,386.5...

UKURASA 8


Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
JE, WAJUA?
Sokwe mtu wapiga 'selfie' DRC
Dhahabu barani Afrika yatoroshwa kila mwaka
Mikakati kuinua ufaulu Mbeya yazaa matunda

UKURASA 13

# JPM afichua mbinu za kuiibia serikali

• **Aeleza** ujanja wa wafanyabiashara kujipatia mabilioni... *Endelea ukurasa 2*



Rais John Magufuli, akikagua maparachichi yanayohifadhiwa kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi, baada ya kuzindua Kiwanda cha Rungwe Avocado Company, wilayani Rungwe, Mkoa wa Mbeya jana. **PICHA: IKULU**

## DC akwepa kitanzi cha Rais soko la madini

UKURASA 3

## Bunge latahadharisha mgomo wa wahadhiri

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA YAIPOTEZA AZAM FC UHURU** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mkurugenzi wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Dk. Agrey Mlimuka (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi rasmi wa Tuzo za Mwajiri Bora kwa mwaka 2019. Kushoto ni Mkuu wa Miradi wa ATE, Joyce Nangai. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JPM afichua mbinu za kuiibia serikali

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli, amesema serikali imeamua kufanya uhakiki wa kodi inayorejeshwa kwa wafanyabiashara baada ya kubaini baadhi yao kuziongeza tarakimu ili wapate malipo makubwa.

Rais Magufuli alifichua mbinu hiyo chafu jana baada ya kutembelea kiwanda cha maparachichi kilichoko Kiwira wilayani Rungwe mkoani Mbeya na mwekezaji wake kuomba serikali impatie kodi hiyo.

Mara baada ya kukitembelea na kukizindua kiwanda hicho, Rais Magufuli alisema walibaini kuwa huko nyuma baadhi ya wafanyabiashara walikuwa wakiandika malipo hewa ili wapate fedha nyingi.

"Malipo ya kodi inayorejeshwa yamekuwa na matatizo, mtu anakuja anawekeza kiwanda, akishawekeza kama amenunua kifaa cha kiwandani kwa Sh. milioni tano anasema Sh. milioni 50, kama alinunua Sh. milioni 50, anasema alinunua Sh. milioni 500 halafu zinakatwa kwenda kudaiwa serikali," alisema.

Rais Magufuli alisema ni kutokana na changamoto hiyo serikali ilikuwa ikilipa malimbikizo ya kodi hewa.

"Tumelaaliwa sana katika kipindi cha nyuma ndiyo maana serikali ikasema lazima tuzikague kodi hizo zote zinazofanyika kama ambavyo wanavyofanya nchi nyingine, ukiwa Ulaya huwezi ukaomba kodi inayorejeshwa ukapewa, lazima wafanye uhakiki kwanza," alisema.

Rais Magufuli alisema hicho ndicho kinachofanywa na serikali yake kwa sasa ili kutoruhusu mianya hiyo kuendelea.

INAENDELEA UK. 8

# Bunge labaini mgomobaridi wa wahadhiri

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limebaini kuwa kuna changamoto ya wahadhiri na watumishi wa vyuo vikuu kutolipwa stahiki zao zikiwamo posho za nyumba.

Limesema hali hiyo imesababisha baadhi ya wahadhiri kuzuia matokeo ya mitihani, kwamba kuna hatari ya kutokea mgomo baridi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Juma Nkamia, ameeleza kuwa kamati hiyo inaishauri serikali kuhakikisha maslahi ya wahadhiri hao na watumishi wa vyuo vikuu, yanatolewa mapema ili kuepuka madhara yoyote ambayo yanaweza kutokea.

Nkamia alikuwa akisoma taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2018/19 jana pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/20.

"Kamati inatambua umuhimu wa elimu ya juu ambapo wahadhiri na watumishi wengine ni nyenzo muhimu katika utoaji wa elimu. Hata hivyo, kamati imebaini kuwa kuna changamoto ya wahadhiri na watumishi hawa wa vyuo vikuu kutolipwa stahiki zao ikiwamo posho ya nyumba.

"Changamoto hii imepelekea baadhi ya wahadhiri kuzuia matokeo ya mitihani, lakini kamati inaona kuna hatari ya kutokea mgomo baridi."

Aidha, alisema kamati hiyo imeelezwa kuwa baadhi ya vyuo vimeshindwa kulipa mishahara ya walimu (wahadhiri), hali iliyosababisha wahadhiri hao kuzuia kutoa matokeo ya mitihani.

Pia, Nkamia amelieleza Bunge hilo kuwa kamati hiyo, licha ya kupongeza juhudi zinazofanywa na Tume ya Vyuo Vikuu nchini (TCU) kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika vyuo nane na kuvifungia kufanya udahili kutokana na mapungufu waliyoyabaini katika utoaji wa elimu, lakini inaona hatua zimechelewa kuchukuliwa hali ambayo imeathiri wanafunzi wengi wasio na hatia kutokana na vyuo hivyo kufungwa.

Ameeleza kuwa kamati hiyo inashauri ili kuepuka kuvifungia vyuo ni vyema TCU ikawa inavifuatilia kwa ukaribu na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vyuo vyote nchini ili kubaini upungufu mapema na kushirikiana nao kufanya maboresho.

# Kampuni yaacha deni la mabilioni

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amesema Kampuni ya Tan Power Resources (TPR) imeacha Sh. bilioni 2.9 iliposititisha shughuli zake kwenye mgodi wa makaa ya mawe wa Kiwira mkoani Mbeya.

Biteko aliyasema hayo Rungwe mkoani Mbeya jana mbele ya Rais John Magufuli baada ya kutakiwa na kiongozi huyo wa nchi kutoa ufafanuzi kwanini mgodi huo haufanyi kazi na utaanza lini.

Biteko alisema mgodi huo ulisimama tangu mwaka 2015 baada ya kampuni hiyo kuondoka na kuurudisha serikalini.

"Changamoto kubwa iliyokuwapo wakati kampuni hiyo ikiondoka iliacha deni ambalo lilipaswa kulipa serikali Sh. bilioni 2.9. Ili kuhamisha ubia kutoka kampuni hiyo ilikuwa lazima deni hilo lilipwe," alisema.

Biteko alisema Rais Magufuli aliwapa maelekezo ya kulifanyia kazi kwa haraka suala hilo kwa kuhamisha hisa asilimia 70 za kampuni hiyo ziende serikalini.

"Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Madini tumeshakaa kuona deni hili linalipwa kwa namna gani. Yapo madeni makubwa ambayo kampuni hii iliyaacha ya jumla ya Sh. bilioni 40.6, madeni ambayo serikali ya awamu ya tano iliyakuta," alisema.

Aliongeza kuwa baada ya madeni hayo kuhakikiwa, yalishuka na kufikia Sh. bilioni 1.24, wanachi 1,862 wakidai lakini baada ya uhakiki, walipungua na kubaki 862.

Waziri Biteko alisema wawekezaji wanaotaka kuwekeza kwenye mradi huo ni wengi lakini changamoto ni kampuni iliyokuwa ikiuendesha, kukimbia baada ya kutafutwa na Mamlaka ya Mapato (TRA).


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 27//04/2019

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **ALHAMIS** tarehe **02/05/2019** kampuni ya **S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR kuelekea **KAGERA** gari hilo lenye namba za usajili:

**T794 DFQ /T 394 ADH .**

2.Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 21.0
Upana - mita 3.24
Kimo - mita 5.20

3.NJia itakayotumika **DAR** hadi **KAGERA** kupitia **MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

# Mitandao ya kijamii yamponza diwani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

DIWANI wa Kata ya Ngokolo Manispaa ya Shinyanga, Emmanuel Ntobi, amefukuzwa kwenye Baraza la Madiwani na kutohudhuria vikao vitatu vya baraza hilo, pamoja na kunyimwa stahiki zake zote kwa kipindi hicho alichosimamishwa kutokana na tuhuma za kuichafua manispaa hiyo kupitia mitandao ya kijamii.

Imedaiwa diwani huyo mara kwa mara amekuwa akiichafua manispaa hiyo kupitia kwenye mitandao ya kijamii kuwa inafanya ufujaji wa fedha kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo, tuhuma ambazo zimedaiwa siyo za kweli kutokana na kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha ukweli huo wa matumizi mabaya ya fedha.

Akisoma taarifa jana ya kamati ya maadili baada ya madiwani hao kujigeuza kamati ya kumjadili diwani huyo kuhusu utovu wake wa nidhamu, Naibu Meya wa manispaa hiyo, John Kisandu, alisema wameazimia kumfukuza ndani ya baraza na kutohudhuria vikao vitatu mfululizo na kukosa stahiki zake zote.

Alisema kwa mujibu wa kanuni za kudumu za halmashauri, mjumbe ambaye atatoa kashfa za kuichafua manispaa na kushindwa kuthibitisha ukweli, achachukuliwa hatua kwa kusimamishwa kuhudhuria vikao vitatu pamoja na kukosa stahiki zake zote ikiwamo posho, nauli na kinga ya matibabu.

"Kanuni ya 28 kipengele cha tatu za kanuni za kuduma za halmashauri (2013) namba mbili, kinasema endapo mjumbe aliyetoa hoja za kashfa akakataa kufuta kauli yake kwa kuomba msamaha kwa maandishi kama alivyoelekezwa na kamati ndogo, meya wa mkutano atamsimamisha mjumbe huyo kuhudhuria vikao vitatu na kunyimwa stahiki zake zote," alisema Kisandu.

Kwa upande wake diwani huyo, Emmanueli Ntobi, alikiri tuhuma ambazo amekuwa akizitoa ni za kweli kuwa manispaa hiyo ya Shinyanga inafanya ufujaji wa fedha kwenye utekelezaji wa miradi yake ya maendeleo, na kubainisha maamuzi yaliyotolewa hakubaliani nayo bali atakwenda kudai haki yake mahakamani.

Aidha, alisema anaiomba serikali kuu iunde tume ya kwenda kuichunguza miradi ya maendeleo ya manispaa ya Shinyanga ambayo inatekelezwa kama haifanyi ufujaji wa fedha, ukiwamo mradi wa machinjio ya kisasa, upimaji wa viwanja pamoja na ujenzi wa kituo cha afya Kambarage.

Naye Katibu Tawala wa Wilaya ya Shinyanga, Boniphace Chambi, aliwataka madiwani wa manispaa hiyo kuacha kuitumia vibaya mitandao ya kijamii kwa kuichafua serikali na kama wanahoja waziseme kwenye vikao vyao vya baraza na zisipo shughulikiwa waende kwenye mamlaka zingine ikiwamo Takukuru.



Wajumbe wa taasisi ya Habari Development Association, kwa kushirikiana na maofisa wa kampuni ya Eastenders Tours and Safaris pamoja na Maofisa wa Manispaa ya Ilala, wakishiriki kufanya usafi katika fukwe za Bahari ya Hindi, eneo la Seaview, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

## Majaliwa aziagiza taasisi uhakiki wa bidhaa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezitaka taasisi zinazofanya uhakiki na upimaji bidhaa nchini zijirekebishe na ziongeze kasi ya utoaji matokeo kwa wateja.

"Kumekuwa na malalamiko kutoka mipakani juu ya bidhaa zinazochukuliwa ili zikapimwe kwamba zinachukua muda mrefu. Tume ya mionzi, TBS na TFDA ni mioyo mwa taasisi zinazolalamikiwa. Tumieni fursa hii kujirekebisha na kuharakisha utoaji wa matokeo," alisema.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo jana wakati akizindua maabara ya kisasa ya Teknolojia ya Nyuklia ya Tume ya

INAENDELEA UK. 8




# DC akwepa kitanzi cha Rais JPM soko la madini

**Na Mary Mosha,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amekikwepa 'kitanzi' cha Rais John Magufuli kwa kuanzisha soko la uuzaji wa madini yakiwamo ya Tanzanite ndani ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Katika makabidhiano ya jengo maalum litakalotumika kuratibu shughuli zote za madini wilayani mwake jana, Ole Sabaya alisema jengo hilo litaanza kutumika kwa shughuli hiyo ndani ya siku saba kuanzia jana.

Ole Sabaya alikabidhiwa jengo hilo na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Usimamizi na Uendeshaji wa Uwanja wa Ndegewa Kia (Kadco), Christopher Mukoma, baada ya kuzungumza nao kuhusu jinsi watakavyotekeleza agizo la Rais Magufuli kuanzisha soko la madini.

Alisema kuwa baada ya taratibu zote kukamilika, Waziri wa Madini atalifungua ili litumike kwa shughuli iliyokusudiwa.

Amewataka Ofisa Madini Mkoa wa Kilimanjaro, Fatma Kiondo, mchakato unaohitajika unafanywa kuhakikisha soko hilo linaanza kufanya kazi.

Alisema kuwa baada ya kupatikana kwa jengo hilo litakalotumika kwa shughuli hiyo kwa muda, wanajipanga kujenga soko la kimataifa la madini na maeneo ya utalii kwenye lango la KIA, ikiwa ni njia mojawapo ya kuongeza watalii na kukuza uchumi wa taifa.

"Soko hilo linatarajiwa kuanzishwa hivi karibuni na tunawaomba wadau mbalimbali wakiwamo wa madini kuhakikisha wanawatangazia watalii juu ya biashara inayofanywa hapo ili kukuza uchumi wa nchi," alisema.

Ole Sabaya aliongeza: "Ndani ya hizo siku saba wataalamu wetu watakuwa tayari kwenye chumba hicho na kutakuwapo na sampuli mbalimbali za madini yote yanayopatikana nchini ili kuwasaidia wafanyabiashara pamoja na watalii katika kupata vitu vyenye ubora unaosimamiwa na serikali."

INAENDELEA UK. 8

TANGAZO

# BENKI YA STANBIC TANZANIA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa | Robo Mwaka/Mwaka uliopita |
|---|---|---|---|
| | | 31-Mar-19 | 31-Dec-18 |
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 9,964 | 14,823 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 152,498 | 132,530 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 71,357 | 69,112 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 61,833 | 119,874 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - 896 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 22,354 | 35,743 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 184,569 | 76,591 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 151,350 | 193,426 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 810,242 | 672,899 |
| 12 | Mali Nyingine | 50,113 | 42,916 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 54,334 | 47,266 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,568,614** | **1,404,282** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 214,917 | 160,352 |
| 18 | Amana za Wateja | 903,165 | 851,380 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 36,173 | 49,911 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 2,477 | 58 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 26 | 26 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 36,652 | 37,608 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 22,354 | 35,743 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 908 | 334 |
| 27 | Dhima Nyingine | 59,161 | 21,745 |
| 28 | Madeni | 18,941 | 18,502 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,294,775** | **1,175,658** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **273,840** | **228,625** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 8,400 | 7,390 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 112,396 | 75,487 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 137,761 | 121,540 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 6,307 | 16,221 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 8,975 | 7,987 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **273,840** | **228,625** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 574,742 | 593,169 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 62,159 | 56,488 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 38,816 | 39,273 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 17.5% | 16.3% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7.3% | 7.9% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 88.3% | 79.8% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 55.6% | 53.3% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79.0% | 72.1% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 4.2% | -1.0% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 11.7% | 10.5% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi |
|---|---|---|---|---|---|
| | TAARIFA | 31-Mar-19 | 31-Mar-18 | 31-Mar-19 | 31-Mar-18 |
| 1 | Mapato ya Riba | 24,421 | 23,138 | 24,421 | 23,138 |
| 2 | Gharama za Riba | 3,845 | 2,862 | 3,845 | 2,862 |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **20,576** | **20,276** | **20,576** | **20,276** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 430 | 1,433 | 430 | 1,433 |
| | **Mapato baada ya tengo katika mikopo** | 20,146 | 18,844 | 20,146 | 18,844 |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **15,970** | **15,156** | **15,970** | **15,156** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 9,857 | 8,469 | 9,857 | 8,469 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 6,065 | 6,488 | 6,065 | 6,488 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 48 | 199 | 48 | 199 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba** | **26,582** | **27,983** | **26,582** | **27,983** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 13,778 | 13,950 | 13,778 | 13,950 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 3,304 | 4,454 | 3,304 | 4,454 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 9,499 | 9,580 | 9,499 | 9,580 |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **9,534** | **6,016** | **9,534** | **6,016** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 3,227 | 2,166 | 3,227 | 2,166 |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **6,307** | **3,850** | **6,307** | **3,850** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| | i) Mabadiliko ya thamani katika amana zinazouzika | 31 | 2,687 | 31 | 2,687 |
| | ii) Kodi ya mabadiliko ya thamani katika amana zinazouzika | - 9 | - 806 | - 9 | - 806 |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **6,328** | **5,731** | **6,328** | **5,731** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 530 | 560 | 530 | 560 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.8 | 1 | 0.9 | 1 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 9 | 9 | 9 | 9 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.4% | 0.3% | 0.4% | 0.3% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.6% | 1.8% | 2.6% | 1.8% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 65.8% | 73.1% | 65.8% | 73.1% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.7% | 2.0% | 1.7% | 2.0% |

*Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho*

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | TAARIFA | 31-Mar-19 | 31-Dec-18 | 31-Mar-19 | 31-Mar-18 |
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **6,307** | **6,423** | **6,307** | 3,850 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 3,260 | 3,827 | 3,260 | 1,922 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | - 123,955 | - 73,491 | - 123,955 | - 12,811 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 24 | - 218 | 24 | - 1 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 79,223 | 100,828 | 79,223 | 23,754 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 39,830 | 62,343 | 39,830 | 43,945 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 43,044 | - 13,383 | 43,044 | 10,343 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | - 16,085 | 8,880 | - 16,085.15 | - 5,173 |
| | - Kodi Iliyolipwa | - 3,590 | - 87 | - 3,590 | - 3,351 |
| | - Mengineyo (bainisha) | - 2,715 | - | - 2,715 | - |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **25,344** | **95,121** | **25,344** | **62,479** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - 1,448 | - 1,690 | - 1,448 | - 1,086 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 33 | 165 | 33 | 9 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | - **1,415** | - **1,525** | - **1,415** | - **1,077** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 37,920 | - | 37,920 | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 439 | - 153 | 439 | - |
| | Mengineyo (bainisha) | 988 | - 742 | 988 | - 5,344 |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | ***39,348*** | - ***895*** | ***39,348*** | - ***5,344*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 63,277 | 92,701 | 63,277 | 56,058 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 272,375 | 174,526 | 272,375 | 170,472 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 335,651 | 267,227 | 335,651 | 226,530 |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mabadiliko thamani katika amana zinazouzika | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ! **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 7,390 | 75,487 | 137,761 | 0 | 5,719 | 2,267 | 228,624 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 6,307 | - | - | - | 6,307 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 22 | 22 |
| Miamala na wanahisa | 1,010 | 36,910 | - | - | - | - | 37,920 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - 10,495 | 10,495 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - 1,372 | - | 1,372 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | 967 | 967 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,400** | **112,396** | **132,201** | **10,495** | **7,091** | **3,256** | **273,840** |
| " **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 7,390 | 75,487 | 131,372 | 2,496 | 4,648 | 4,463 | 225,855 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 16,221 | - | - | - | 16,221 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - 2,448 | - 2,448 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1,424 | - 2,496 | 1,072 | - | - 0 |
| Mengineyo | - | - | - 11,256 | - | - | 253 | - 11,003 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **7,390** | **75,487** | **137,761** | **0** | **5,719** | **2,267** | **228,624** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2019**

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| Ken Cockerill **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | | 29-Apr-19 |
| Lydia Kokugonza **(Mkuu wa Fedha)** | | 29-Apr-19 |
| Jonathan Ngoma **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | | 29-Apr-19 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| 1. Prof. Marck Mwandosya **(Mwenyekiti wa bodi)** | | 29-Apr-19 |
| 2. Nada Margwe **(Mjumbe wa bodi)** | | 29-Apr-19 |

215203102

TANGAZO

# STANBIC BANK TANZANIA

## DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2015
## MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

| No. | Item/Transaction | Charges/Fees<br>TZS | <br>USD |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Current Accounts** | | |
| a) | Required Minimum balance | 0 | 0 |
| b) | Monthly Service/Management Uhuru Banking | FREE | FREE |
| c) | Monthly Service/Management Private banking PAYT | 29,500 | 17.70 |
| d) | Monthly Service/Management Fees Private banking Bundle | 53,100 | 31.86 |
| e) | Monthly Service/Management Fees Biashara Direct segment | 22,000 | 13.20 |
| f) | Monthly Service/Management Fees Sole propriator segment | 15,000 | 10.62 |
| g) | Monthly Service/Management Fees SME banking segment | 35,400 | 21.24 |
| h) | Monthly Service/Management Fees Commercial banking segment | 64,900 | 38.94 |
| i) | Monthly Service/Management Fees Non commercial Entities | FREE | FREE |
| j) | Monthly Service/Management Fees Corparate Banking | 33,040 | 12.98 |
| k) | Over the counter withdrawal fee(per segment and price option) | TZS 3,894 for amounts below 20M,<br>0.15% of value for amount above 20M<br>max 118,000 | For FCY withdrawals - 1.18% min 7.08,<br>Maximum US$300 |
| l) | ATM withdrawal fee own ATM Private banking | 900 | 0.60 |
| m) | ATM withdrawal fee own ATM Uhuru Banking | 950 | 0.83 |
| n) | ATM withdrawal fee other banks (local) Uhuru banking | 1,000 - 400,000 =2,800<br>400,001-above=4,000 | 1,000 - 400,000 =2.8<br>400,001-above=4 |
| o) | ATM withdrawal fee other banks (local) Private Banking | 1,000 - 50,000 =1,200<br>50,001 - 200,000 = 1,900<br>200,001 - 400,000 = 2,800<br>400,001-above=4,000 | 1,000 - 50,000 =1.2<br>50,001 - 200,000 = 1.9<br>200,001 - 400,000 = 2.8<br>400,001-above=4 |
| p) | ATM withdrawal fee /nternational | 8,000 | 5.00 |
| q) | ATM Mini Statement | 900 | 0.60 |
| r) | Interim Statement per page | 4,720 | 2.36 |
| s) | Periodic schedule statement | FREE | FREE |
| t) | Issue of cheque book | 413 per leaf | 0.36 per leaf |
| u) | Returned updaid Cheque( insuficient fund) | 100,000 | 60.00 |
| v) | Special Clearance | 47,200 | 28.32 |
| w) | Counter Cheque | 14,160 | 8.26 |
| x) | Stop Payment | 47,200 | 28.32 |
| y) | Salary processing to staff banking with STB(SFI) | 4,000 | 0.60 |
| z) | Salary processing to staff banking with STB(Manual) | 4,000 | 2.40 |
| aa) | Salary processing to staff banking with other bank(EFT) | 4,000 | 1.80 |
| ab) | Salary processing to staff banking with other bank(TISS) | 10,000 | Equivalent of 10 000 |
| ac) | Standing Order to 3rd partywithin stanbic | 4,720 | 2.36 |
| ad) | Standing Order to other banks local | 33,040 | 17.70 |
| ae) | Standing Order own account | FREE | FREE |
| af) | Balance enquiry (Over the counter) | 4,720 | 2.36 |
| ag) | ATM card issuance | FREE | FREE |
| ah) | ATM card replacement/Renewal | 25,000 | 15.00 |
| ai) | Unarranged Overdraft | 100,000 | 60.00 |
| aj) | Overdrawn Account interest charge | 36% | 21% |
| ak) | Interbank Transfer Normal | 3,000 | 1.80 |
| al) | Interbank Transfer Express (TISS) | 10,000 | Equivalent of 10 000 |
| am) | Interbank Transfer | 33,040 | 17.70 |
| an) | Bill Payments through non branch channels( E channel) | FREE | FREE |
| ao) | Deposit fee | FREE | FREE |
| **2.0** | **Savings Accounts** | | |
| a) | Required minimum opening balance | 50,000 | 100.00 |
| b) | Monthly service fee (if balance breach minimum balance required) | 2,000 | 1.18 |
| c) | Interim statement | | FREE |
| d) | Account closure | FREE | FREE |
| **3.0** | **Electronic banking** | | |
| a) | Internet banking monthly fee | FREE | FREE |
| b) | Internet transfers within own accounts STB | FREE | FREE |
| c) | Internet transfers 3rd party transfer STB | 1,000 | 0.60 |
| d) | Internet transfers other banks normal(EFT) | 2,000 | 1.20 |
| e) | Internet transfers other banks express(TISS) | 8,000 | Equivalent of 8 000 |
| f) | Bank to wallet Private Banking | 1,000 - 50,000 =1500<br>50,001 - 200,000 = 2000<br>200,001 - 300,000 = 2500<br>300,001-500,000=3000<br>500,000-1,000,000=3,500 | Equivalent |
| g) | Bank to wallet Uhuru Banking | 1,000 - 25,000 =1500<br>25,001 - 100,000 = 2000<br>100,001 - 250,000 = 2500<br>250,001-500,000=3000<br>500,000-1,000,000=3,500 | Equivalent |
| h) | Balance and statement | FREE | FREE |
| i) | Air time top up | FREE | FREE |
| j) | SMS Banking | FREE | FREE |
| k) | Till to bank | 1.5% of the amount | 1.5% of the amount |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowlwdge and information

Signed by:

| | | |
|---|---|---|
| **Chief Executive Officer** | **K. Cockerill** | ............................................... |
| **Head, Personal and Bussiness Banking** | **Ndadzungira, Brian B** | ............................................... |
| **Head, Corporate and Investment Banking** | **Manzi Rwegasira** | ............................................... |

| No. | Item/Transaction | Charges/Fees<br>TZS | <br>USD |
|---|---|---|---|
| **4.0** | **Foreign Exchange Transactions** | | |
| a) | Purchase/Sale of TC's ttransactions over the counter | N/A | 1.475% min 43.66 |
| b) | Purchase of foreign cheque | 1.18% of the amount min 100 000, | 1.18% of the amount min 59, Max 236 |
| c) | Telegraphic transfer Inward | N/A | 0.25% Min $11 Max $35 |
| d) | Telegraphic transfer Outward | N/A | 0.295%. Min $50, Max 150 |
| | Telegraphic transfer Outward( For TT done from TZS accounts) | N/A | $59 |
| e) | TISS outward | 10,000 | 10 000 Equivalent |
| | 0.826 | | |
| f) | TISS inward | FREE | FREE |
| g) | Cancellation of TT/Recall of funds | N/A | $75 |
| **5.0** | **Personal Loan** | | |
| a) | Processing/ Arrangement/ Appraisal fee | | |
| | (i) Personal Loans | 2.00% | 2.00% |
| | (ii) Overdrafts | 2% of the facility min 100 000. | 2% of the facility min $100 |
| | (iii) Mortgage Finance | 1.18% | 1.18% |
| | (iv) Asset Finance | 1.18% | 1.18% |
| b) | Early repayment | 3.0% | 3.0% |
| | Valuation fees | As per valuer | As per valuer |
| **6.0** | **Other Disclosures (Viambatanisho Vinginevyo)** | | |
| | Base/Prime Lending Rate | 21% | 9% |
| | Maximu spread over Base/Prime lending rate | 4.5% | 2% |
| **7.0** | **Deposit Rate (*subject to change from time to time*)** | | |
| | a) Fixed Deposits | | |
| | **TZS** | **+1BN** | **+1M** |
| | 1month | 1.25% | 0.05% |
| | 3months | 1.45% | 0.10% |
| | 6months | 1.90% | 0.15% |
| | 9months | 2.80% | 0.20% |
| | 12months | 3.70% | 0.25% |
| | b) Savings Account | 3.00% | 0.20% |
| | c) Current Account | Nil | Nil |
| **8.0** | **Trade Finance** | | |
| | a) Letters of Credit/Guarantee | | |
| | Establishment Fee - per quarter | Nil | 1% on establishment per quarter and part thereoff min $300 |
| | b) Documentary collection( clean bill) | Nil | $150 |

215203102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Serikali ilifanyie kazi hili la Kardinali Pengo

**MOJA** ya maelekezo aliyoyatoa Rais John Magufuli kwa viongozi wapya aliowateua hususan wakuu wa mikoa na wilaya baaada ya kuingia madarakani ni kuwasimamia kwa dhati wananchi kufanya kazi katika maeneo yao.

Aliwaelekeza viongozi hao kuwachukulia hatua ikiwamo kuwakamata vijana ambao wanacheza mchezo wa pool asubuhi, badala ya kufanyakazi, ambayo ndio msingi wa kujiletea maendeleo.

Rais Magufuli alisema watu wa aina hiyo ikiwezekana wakamatwe na kupelekwa kwenye makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kushiriki katika shughuli za uzalishaji.

Alisema hivyo kwa kuamini kuwa taifa ambalo wananchi wake hawafanyi kazi haliwezi kuendelea wala kujitegemea na linaweza kuwa taifa la watu ombaomba na tegemezi, ambayo ni sifa mbaya sana kwa watu wanaojitambua.

Msisitizo huo wa watu kufanyakazi unatokana na kaulimbiu yake wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu ya 'Hapa kazi tu'.

Hata hivyo, maneno yaliyozungumzwa Jumapili na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, ya kukemea ulevi asubuhi, yanatoa ishara kwamba baadhi ya wananchi hawajalipa umuhimu suala la kufanyakazi.

Kardinali Pengo mbali na kukemea ulevi wa asubuhi, akitaka serikali kuchukua hatua dhidi ya wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Askofu Pengo alitoa rai hiyo Jumapili katika misa ya kumsimika Askofu Gervas Nyaisonga kuwa Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya.

Katika ibada hiyo iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa akiwamo Rais John Magufuli, Askofu Pengo alisema ni serikali pekee inayoweza kuwawezesha kutamka kwa dhati kuwa haiwezekani watu kuwa wamelewa kabla ya saa tatu asubuhi.

Alisema kanisa halina mahali pa kuwachukua vijana na likawaweka na kuwapa nidhamu ya kutokulewa kabla ya saa tatu asubuhi.

Alisema Askofu hatakiwi kubeza shughuli inayofanywa na serikali ya kuwapa nidhamu vijana hao na kueleza kuwa kwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha Roho Mtakatifu.

Kauli ya Kardinali Pengo ina ujumbe mzito kwa jamii yetu, hivyo inahitaji tafakuri na kufanyiwa kazi, kwa lengo la kuwarejesha vijana katika mstari.

Tunasema kuwa kiongozi huyo wa kiroho ametoa kauli yenye ujumbe mzito na muhimu kwa jamii, kwa kuwa viongozi hao wa dini wanaishi karibu kabisa na jamii.

Viongozi hao kwa kuishi karibu na jamii, wanaelewa mambo mengi ya makundi yote ya kijamii, zikiwamo changamoto zonazoikabili.

Kwa hiyo, kuamua kwake kueleza hayo hadharani tena mbele ya kiongozi mkuu wa nchi, ina maana ameguswa na na mwenendo huyo wa vijana, ambao hautoi mwelekeo wa jamii yetu katika miaka ijayo.

Hata hivyo, bado tunaona kuwa jukumu la kulipatia ufumbuzi suala la vijana kulewa asubuhi ambao ni wakati wa kufanyakazi ni la serikali kwa kushirikiana na makundi mengine katika jamii, wakiwamo wazazi na viongozi wa dini.

Serikali inaweza kutumia sheria kuwabana, huku makundi mengine yakiwa na jukumu la kuwafundisha vijana nidhamu na maadili mema.

Tukumbuke kuwa kuliacha suala la ulevi, tunakuwa tunawaacha vijana wetu kujiingiza katika vitendo vingine vya kihalifu kwa kuwa ulevi ni lichocheo kikuu.

Tunampongeza Kardinali Pengo kwa kutonyamaza kimya, huku tukiamini kila mmoja atatimiza wajibu wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Raphael Kibiriti

# Mamlaka za miji zichukue somo la usafi Stendi ya Mizengo Pinda

**KUNA** faida nyingi za usafi kwa mtu binafsi, kijiji, mji, jiji, taifa na dunia kwa ujumla wake.

Afya ni moja ya faida hizo, kitu chenye thamani kubwa kwa maisha ya binadamu kwa sababu afya zetu zinapokuwa timamu ndiyo mtaji mkuu katika dhima nzima ya kujenga ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla wake.

Lakini suala la usafi haliishii kwa binadamu tu, bali hata kwenye mazingira anayoishi.

Kwa mfano mazingira yenye taka ambazo hazizolewi, zilizolalala barabarani au katika mapipa ya taka yasiyofunikwa ni chanzo cha kuzalisha vimelea na wadudu na hivyo magonjwa ya kila aina yakiwamo ya kuambukiza kama vile kipindupindu.

Moja ya vitu vilivyo ndani ya uwezo wetu ambavyo tunaweza kuvifanya kwa uhakika na vikawezekana kwa maana ya kutohitaji msaada kutoka nje ni cha kuweka maeneo yetu, makazi yetu, miji yetu katika hali ya usafi.

Muungwana anasema hili linawezekana baada ya kuwa ametembelea Stendi Kuu ya Mizengo Pinda iliyoko mjini Mpanda, katika mkoa wa Katavi.

Ilikuwa Machi mwaka huu wakati alipoenda kusalimia ndugu na jamaa katika maeneo hayo.

Muungwana alifika Stendi Kuu ya Mizengo Pinda akitokea Stendi ya Treni ya Mpanda kwa usafiri wa Bodaboda, ikiwa ndiyo mara yake ya kwanza kufika katika mji huo.

Wakati aliposhushwa na bodaboda kwenye lango kuu la kuingilia stendi hiyo, alitahadharishwa na dereva wa usafiri huo kwamba kama ni mara yake ya kwanza kufika katika stendi hiyo, basi achukue tahadhari.

Achukue tahadhari ya kutotupa uchafu wowote ule uwe ni wa maganda ya pipi, matunda, chupa za maji au mwingine, zaidi ya kwenye mapipa ya taka yaliyoko sehemu mbalimbali ndani ya stendi hiyo.

Aidha, akaelezwa kwamba stendi hiyo ina njia zilizo maalumu kwa ajili ya watu kupita na pia ina sehemu zilizopandwa nyasi na maua kwa ajili ya kutunza mandhari, hivyo apite kwenye njia zilizoruhusiwa.

Kwamba akikatisha kwingine zaidi ya kwenye njia hizo kama ilivyo 'ada' kwa Watanzania wa maeneo mbalimbali nchini ambao hupita hata katika njia au maeneo yasiyoruhusiwa, basi atakamatwa na kukabiliwa na mkono wa sheria ikiwamo faini ya Sh. 50,000.

Baada ya kuingia ndani ya stendi, mandhari ya kuvutia na usafi ulivyo ulimfanya Muungwana aamini alichoambiwa na dereva wa bodaboda.

Karibu abiria wote na wananchi wanaoitumia stendi hiyo wakiwamo wafanyabiashara wa matunda na wenye biashara zingine kama za maduka, na za 'kimachinga' walionekana kuwa wastaraabu wakizingatia kanuni zote za usafi zilizoelekezwa.

Aidha, Muungwana alishuhudia askari walioajiriwa kusimamia sheria na kanuni za usafi ndani ya stendi hiyo, wakiwa kazini karibu katika kila eneo la stendi hiyo wakiwa macho kuhakikisha hakuna mtu asiyekiuka sheria na kanuni za usafi za stendi hiyo.

Alipata pia fursa ya kutumia huduma ya vyoo vilivyoko katika stendi hiyo ambavyo ni visafi kutokana na wanaoviendesha kutimiza wajibu wao kikamilifu.

Mpaka anaondoka katika stendi hiyo majira ya saa sita mchana kutokea saa kumi na mbili asubuhi kuelekea kwa ndugu na jamaa zake, bado hali ya usafi ilikuwa ya juu na mazingira yake yakiwa ya kuvutia.

Hali hiyo iliacha swali la kujiuliza kwa Muungwana kwamba kwa nini Stendi ya Mizengo Pinda imeweza, wakati stendi zilizo nyingi nchini zinashindwa?

Ni rai basi ya Muungwana kwa stendi zilizoko katika miji na majiji mengine hasa jiji la Dar es Salaam, wakaitembelea stendi hiyo inayoendeshwa na Manispaa ya Mpanda kujifunza mafanikio yake.

Ninasema hivyo nikiwa ninajua hali ilivyo katika Stendi Kuu ya Ubungo, na zingine kama zile za Mawasiliano, Makumbusho, Kariakoo, Mbagala, Mbezi Mwisho...kwa kuwa ni mkazi wa jiji hili.

# TANGAZO

DTB DIAMOND TRUST BANK

Achieve More

## VIWANGO VYA TOZO NA ADA ZA HUDUMA ZETU- 2019

### KUTOA FEDHA - TZS

| | |
|---|---|
| Akaunti za Akiba | |
| A. Zaidi ya 500,000 | BURE |
| B. Chini ya 500,000 | TZS 750 |

### ADA ZA MALIPO

#### KUPOKEA FEDHA

| | |
|---|---|
| Kupokea fedha kwa njia ya TISS | BURE |

#### KUTUMA FEDHA

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| Kwa njia ya TISS | TZS 10,000 | USD 10 |
| Kwa njia ya EFT | TZS 3,500 | - |
| Kwenda nje ya nchi | - | USD 45 |
| Ndani ya Benki - DTB | BURE | BURE |

#### KIMA CHA CHINI CHA KUFUNGULIA AKAUNTI

| | | |
|---|---|---|
| Akaunti ya hundi | TZS 50,000 | USD 100 |
| Akaunti ya Akiba | | BURE |

#### KUFUNGA AKAUNTI

| | | |
|---|---|---|
| Akaunti ya Hundi | TZS 30,000 | USD 30 |
| Akaunti ya Akiba | TZS 15,000 | USD 15 |
| Akaunti ya Smart Saver | | BURE |
| Akaunti ya Hundi - Premium | TZS 23,600 | USD 13 |
| Akaunti ya Akiba ya Prime (EURO, GBP & USD) | | EURO, GBP USD 1 |

#### MAELEKEZO MAALUMU YA KUHAMISHA FEDHA - STANDING INSTRUCTIONS

| | |
|---|---|
| Kwenda akaunti nyingine ndani ya DTB | TZS 2,500 |
| kwenda nje ya DTB | TZS 10,000 |

#### TAARIFA YA AKAUNTI

| | | |
|---|---|---|
| Taarifa ya akaunti kila mwezi | | BURE |
| Taarifa ya akaunti ya kielektroniki | | BURE |
| Taarifa ya akaunti ya mwaka huu | USD 5 | TZS 10,000 |
| Taarifa ya akaunti ya mwaka uliopita | USD 5 | TZS 10,000 |

#### TOZO ZA KADI ZA ATM

| | |
|---|---|
| Ada ya Mwaka | TZS 3,000 |
| Kubadilisha kadi | TZS 10,000 |
| Kuomba namba mpya ya siri | TZS 3,000 |
| Kadi isipochukuliwa kwa muda wa miezi 2 na kuharibiwa | TZS 10,000 |
| Kadi iliyozuiwa kwenye ATM za DTB | TZS 1,000 |
| Kutoa fedha kwenye ATM za DTB | TZS 750 |
| Kutoa pesa kwenye ATM - Benki nyingine | TZS 3,000 |
| Kutoa pesa kwenye ATM - Nje ya nchi | TZS 5,000 |
| Akaunti ya wanafunzi - Kisomi Zaidi | TZS 150 |

#### SALIO KWENYE AKAUNTI

| | |
|---|---|
| Akaunti ya akiba - DTB Super Value | TZS 100,000 |
| Akaunti ya akiba - Premium | TZS 500,000 |
| Akaunti ya Hundi - Standard | TZS 50,000 |
| Akaunti ya Hundi - Standard | USD 100 |
| Akaunti ya Hundi - Premium | TZS 1,000,000 |
| Akaunti ya Hundi - Prime (Fedha za Kigeni) | USD 250 |
| Akaunti ya akiba - DTB Value | TZS 0.00 |
| Akaunti ya akiba - DTB Super Salary | TZS 0.00 |
| Akaunti ya Mwanafuzi - Kisomi Zaidi | TZS 5,000 |
| Akaunti ya Akiba - Standard | TZS 5,000 |
| Akaunti ya Akiba - Prime (Fedha za Kigeni) | USD 25 |

#### TOZO YA KUWEKA FEDHA ZA KIGENI KWENYE AKAUNTI

| | |
|---|---|
| Kuweka fedha chini ya USD/EUR/GBP 50 | 5% |

#### ATM

| | |
|---|---|
| Taarifa fupi ya akaunti | BURE |

#### TOZO YA KUTOA FEDHA - USD

| | |
|---|---|
| Akaunti ya Akiba - (USD 1 mpaka USD 10,000) | BURE |
| Akaunti ya Akiba - (zaid ya USD 10,000) | 0.5% |
| Akaunti ya Hundi - (USD 1 mpaka USD 10,000) | 0.5% |
| Akaunti ya Hundi - (zaidi ya USD 10,000) | 1% |

#### TOZO ZA MIAMALA

| | | |
|---|---|---|
| Akaunti ya Akiba | | BURE |
| Akaunti ya Hundi - Premium | | TZS 500 |
| Akaunti ya Hundi - Standard | USD 0.10 | TZS 300 |
| Kupitisha mishahara | USD 0.50 | TZS 100 |

#### TOZO ZA HUDUMA ZA KILA MWEZI

| | |
|---|---|
| Akaunti ya Akiba - Standard | BURE |
| Smart Saver, Kisomi Zaidi, Amani, Faraja | BURE |
| Akaunti ya Hundi - Standard | TZS 10,000 |
| Akaunti ya Hundi - Premium | TZS 15,000 |

#### RIBA ZA MIKOPO

| | |
|---|---|
| TZS | 20% |
| USD | kiwango cha chini ni 8%; tozo la riba linategemeana na kiwango cha miezi sita ya soko la LIBOR |

#### RIBA YA AMANA ZA MUDA MAALUMU

| Muda | USD > 50,000 | Hadi USD 50,000 | GBP | EUR |
|---|---|---|---|---|
| Mwezi 1 | 0.25% | 0.25% | 0.00% | 0.00% |
| Miezi 2 | 0.25% | 0.25% | 0.00% | 0.00% |
| Miezi 3 | 0.50% | 0.50% | 0.00% | 0.00% |
| Miezi 6 | 0.75% | 0.75% | 0.25% | 0.00% |
| Mwaka 1 | 3.00% | 2.25% | 0.50% | 0.00% |
| Miaka 2 | 3.25% | 2.50% | 0.75% | 0.00% |

#### TOZO NA ADA ZETU KWA NJIA YA MTANDAO (INTERNET)

| | | |
|---|---|---|
| Tozo la tokeni | USD (Tozo sawa na TZS 120,000) | TZS 120,000 |
| Ada ya kila mwezi ya huduma ya intaneti | | TZS 2,000 |
| Ada ya kutengeneza namba ya siri | | TZS 4,000 |
| Ada ya kutengeneza namba ya siri kama umesahau | | TZS 5,000 |
| Kuhamishaji fedha kwa njia ya TISS | | TZS 10,000 |
| Kuhamisha fedha kwa njia ya TT (nje ya nchi) | | TZS 120,000 |

#### ADA YA HUDUMA YA KIBENKI YA NJIA YA SIMU ZA MKONONI (MOBILE BANKING)

| Huduma | Akaunti ya TZS | Akaunti ya USD |
|---|---|---|
| Kupata taarifa fedha inapotoka kwenya akaunti | Haitozwi | Haitozwi |
| Kupata taarifa fedha inapowekwa kwenye akaunti | TZS 50 | USD 0.10 |
| Siku / Wiki / Mwezi | TZS 50 | USD 0.10 |
| Maulizo | Haitozwi | Haitozwi |
| Ada ya kuhamisha fedha | TZS 1000 | Haitozwi |
| Kununua muda wa maongezi | Haitozwi | Haitozwi |
| Huduma ya kukumbushwa kwa ujumbe | Haitozwi | Haitozwi |
| Ada ya kila mwezi - huduma kwa njia ya simu | TZS 250 | USD 0.25 |
| Ada ya namba ya siri | TZS 2,500 | USD 1 |
| Huduma ya malipo kwa njia ya simu | Haitozwi | Haitozwi |
| Kuhamisha fedha kwenda akaunti nyingine ya DTB | Haitozwi | Haitozwi |
| Kuhamisha fedha kwenda kwenye simu na kutoka kwenye simu kwenda kwenye akaunti | TZS 1,000 | USD 1 |

#### TOZO YA HUNDI

| | |
|---|---|
| Tozo la hundi | |
| A. Vitabu vya hundi - TZS | |
| kurasa 25 | TZS 12,500 |
| kurasa 50 | TZS 25,000 |
| kurasa 100 | TZS 50,000 |
| B. Vitabu vya hundi - USD | |
| kurasa 25 | USD 7.5 |
| kurasa 50 | USD 15 |
| kurasa 100 | USD 30 |
| Tozo ya hundi ya benki (kwa matumizi ya akaunti ya hundi tu) | TZS 10,000 |
| Ombi la kusimamisha malipo | TZS 50,000 |
| Tozo ya hundi iliyorudishwa bila malipo | TZS 100,000 |
| Hundi iliyorudishwa | TZS 50,000 |
| Hundi iliyokataliwa na benki nyingine | TZS 25,000 |
| Tozo ya kulipia hundi | TZS 150 |

#### RIBA YA AMANA ZA MUDA MAALUMU - SHILINGI YA TANZANIA

| Kiasi (TZS '000'000) | Call Deposits | Mwezi 1 | Miezi 3 | Miezi 6 | Miezi 12 | Miezi 24 | Miezi 36 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mpaka 200 | 0.0% | 0.75% | 1.25% | 2.75% | 6.00% | 6.25% | 8.00% |
| > 200 - 500 | 0.0% | 1.00% | 1.50% | 3.00% | 6.25% | 6.50% | 8.00% |
| > 500 -1000 | 0.50% | 1.25% | 1.75% | 3.25% | 6.50% | 6.75% | 8.00% |
| > 1000 to 2000 | 0.75% | 1.50% | 2.00% | 3.50% | 6.75% | 7.00% | 8.00% |
| Kwa fedha zaidi ya Bilioni 2 za Kitanzania wasiliana na Mkuu wa Kitengo cha Hazina DTB | | | | | | | |

**NB: Ada na tozo hazijumlishi kodi ya ongezeko la thamani**

#### NJIA ZA KUTUMIA KUWASILISHA MALALAMIKO ENDAPO HUJARIDHISHWA NA HUDUMA ZETU

Mteja ni muhimu katika shughuli zetu, na jukumu letu kuhakikisha kwamba tunakidhi mahitaji yake wakati wote. Endapo utakuwa hujaridhishwa na huduma zetu tafadhali wasiliana nasi kwa njia zifuatazo;

1. Kutana na Meneja wa Tawi husika na wasilisha tatizo ulilonalo kwa mazungumzo au kwa maandishi.
2. Wasilisha malalamiko yako katika kisanduku cha maoni kilichopo ndani ya tawi
3. Tuma barua pepe kwenda: customercare@diamondtrust.co.tz
4. Unaweza pia kuwasilisha malalamiko moja kwa moja kwa uongozi wa ngazi za juu kama ifuatavyo;

Chief Executive Officer at ceo@diamondtrust.co.tz
Chief Operating Officer at coo@diamondtrust.co.tz
Head-Operations at headoperations@diamondtrust.co.tz
Head-Compliance at headcompliance@diamondtrust.co.tz

5. Piga simu namba +255 22 211 4891/2 or +255 699 839 999 or 0800 110 110

Tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kukupatia suluhisho ndani ya siku 2 za kazi, au kwa siku zisizozidi 15 kuanzia tulipopokea malalamiko yako. Tutakupa mrejesho wa hatua zinazochukuliwa kutatua tatizo lako.

Endapo hutoridhishwa na hatua zilizochukulia na benki, tafadhali jaza Form No. 1 inayopatikana katika matawi yetu yote na wasilisha malalamiko yako kwa njia ya barua pepe, kwa mkono, kwa njia ya posta au kwa nukushi kwenda Benki Kuu ya Tanzania kwa anuani ifuatayo;

**Complaints Resolution Desk,**
**Office of the Secretary to the Bank, Bank of Tanzania,**
**2 Mirambo Street,**
**P.O.Box, 11884**
**Dar es salaam.**

215198601

DTB Tanzania DTB Tanzania DTB Tanzania www.dtbafrica.com

# Wizara ya Elimu yataja vipaumbele 15

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imewasilisha bungeni bajeti yake ya zaidi ya Sh. trilioni 1,386.5 huku ikitangaza maeneo 15 ambayo itayapa kipaumbele katika mwaka ujao wa fedha.

Vipaumbele hivyo ni pamoja na kuendeleza elimu ya awali, msingi na sekondari kwa kutoa ithibati ya mafunzo ya ualimu na maendelezo ya kitaalamu ya walimu, kusimamia uendelezaji wa mafunzo katika vyuo vya maendeleo ya wananchi, kutunga na kutekeleza sera za elimu, utafiti,huduma za maktaba,sayansi,teknolojia na ubunifu.

Akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2019/20, Naibu Waziri wa Elimu, William Ole Nasha, aliyataja maeneo mengine ya kipaumbele ni kuainisha mahitaji ya nchi katika ujuzi na kuendeleza, kusimamia ithibati na uthibiti ubora wa shule na vyuo vya ualimu na ithibati ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

Alisema maeneo mengine ni uthibiti ubora wa shule na vyuo vya ualimu, usimamizi wa elimu ya msingi, usimamizi wa elimu maalum, usimamizi na uendelezaji wa elimu ya juu na usimamizi wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

Mengine ni usimamizi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali watu na usimamizi wa rasilimali za wizara.

Ili kutekeleza vipaumbele hivyo, Ole Nasha amelieleza Bunge kuwa malengo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2019/20 ni kujielekeza zaidi kushughulikia programu ya maendeleo ya sekta ya elimu (programu ya lipa kulingana na matokeo katika sekta ya elimu-EP4R).

**MIKOPO ELIMU YA JUU YAONGEZEKA**

Ole Nasha alisema katika mwaka wa fedha 2019/20 Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu imepanga na kutoa mikopo kwa wanafunzi 128,285 ambao ni sawa na ongezeko la asilimia 4.5 ikilinganishwa na mwaka uliopita wa 2018/19.

Kati ya hao, wanafunzi 45,485 watakuwa ni wa mwaka wa kwanza ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.3 ikilinganisha na wanafunzi 41,234 wa mwaka 2018/19.

Aidha, Ole Nasha alisema, "Bodi hiyo itakusanya Sh.bilioni 221.5 kutoka kwa wanufaika ambao mikopo yao imeiva. Hili ni ongezeko la asilimia 40.5 ukilinganisha na mwaka 2018/19 ambao ni Sh. bilioni 157.7"

**SHULE 16 KUANZA KUJIFUNZA KICHINA**

Pamoja na mambo mengine, Ole Nasha ambaye aliwasilisha hotuba hiyo kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema katika mwaka wa fedha 2019/20, Taasisi ya Elimu Tanzania inatarajia kuandika muhtasari wa lugha ya Kichina kidato cha tano na sita ambayo inafundishwa katika shule za sekondari 16.

Alisema shule za sekondari zinazofundisha Kichina ni Zanaki, Benjamini Mkapa, Morogoro, Kilakala, Dodoma, Umonga, Kiwanja cha Ndege, Ilboru, Arusha, Lindi, Pamba, Mkonge, Mbeya, Samora, Old Tanga na Usagara.



Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Kanda ya Dar es Salaam na Pwani, George Lugata (wa tatu kushoto) na Mirza Ngoshani (wapili kushoto) wakikata utepe kuzindua duka jipya la Vodacom katika jengo la Aura jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**.

## Majaliwa aziagiza taasisi uhakiki wa bidhaa

INATOKA UK 3

Nguvu za Atomiki (TAEC) iliyopo Njiro, jijini Arusha.

"Nafahamu kuwa hii Tume inafanya kazi kwa karibu na bandari vituo vya mipakani ili kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini. Naamini kuanzia sasa mtaharakisha upimaji wa bidhaa na vifaa na kutoa majibu ya vipimo haraka," alisema.

Aliitaka Bodi na Menejimenti ya Tume, waendelee kubuni na kuibua miradi mingine zaidi ya matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia.

"Angalieni uwezekano wa kuanzisha kinu cha utafiti kinachotumia teknolojia ya nyuklia (Research Reactor); mtambo wa kuongeza thamani na ubora wa vitu mbalimbali ikiwamo matunda na mazao mbalimbali (multi-purpose irradiator); na mtambo wa kuzalisha dawa za kuchunguza na kutibu maradhi ya saratani (accelerator)."

Amesema kwa kufanya hivyo, maabara hiyo na watumishi wake wataongeza mchango wa teknolojia ya nyuklia kwenye ustawi wa jamii na ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Amesema anatambua kwamba Tume ya Nyuklia Tanzania inakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo uhaba wa wafanyakazi na ufinyu wa bajeti ya ujenzi wa maabara awamu ya pili. "Serikali inazichukua changamoto hizo na itaendelea na juhudi za kuzitafutia ufumbuzi kadiri hali ya kiuchumi itakavyoruhusu," alisema.

Waziri Mkuu aliishukuru Jumuiya ya Ulaya kwa msaada wa vifaa vya maabara hiyo vyenye thamani ya Euro milioni 2.2 (sawa na Sh. bilioni 7.5) na kwamba Serikali itaendelea kuwapa ushirikiano katika sekta mbalimbali.

## JPM afichua mbinu za kuiibia serikali

INATOKA UK 2

Hata hivyo, Rais Magufuli alimwahidi mwekezaji wa kiwanda hicho cha maparachichi kuwa serikali italifanyia kazi suala lake la malipo ya kodi kwa utofauti ili alipwe.

Akiwa eneo hilo, Rais Magufuli pia alitoa Sh. milioni mbili ukiwa ni mchango wake kwenye Shule ya Msingi ya Ilembe kuweka umeme na kununua mashine ya kuchapisha na kumwagiza mbunge wa jimbo hilo kununua mashine hiyo ndani ya siku tano.

"Nachangia Sh. milioni moja kwa ajili ya kutandaza nyaya za umeme kwenye shule hii halafu wewe mhandisi najua mnahitaji nguzo ili kusogeza umeme pale, sasa Sh. 500,000 zitumike kuvuta umeme na zilizobaki kwa ajili ya kutandaza umeme, mwalimu wa shule nakukabidhi Sh. milioni moja mkaongezee kwenye mashine ya photocopy," Rais aliagiza.

## DC akwepa kitanzi cha Rais JPM soko la madini

INATOKA UK 3

Mwishoni mwa wiki, Rais Magufuli, akiwa katika ziarani wilayani Chunya mkoani Mbeya, alitoa onyo kwa wakuu wa mikoa na wilaya ambayo ina madini, lakini hadi sasa hawajatekeleza agizo lake la kuanzisha masoko ya madini.

Rais Magufuli alisisitiza kuwa hawezi kuwa na wakuu wa mikoa wanaoshindwa kutekeleza maagizo yake. Alisema kwake ukuu wa mkoa ni kufanya kazi ya kuwatumikia wanyonge na si vinginevyo.

Ofisa Mwandamizi wa Madini Mkoa wa Kilimanjaro, Fatma Kiondo, akizungumzia soko la madini, alisema watahakikisha wanatekeleza agizo hilo kwa muda uliopangwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

"Tutawasiliana na tume pamoja na wizara kufikisha wazo hilo ili kuhakikisha tunafungua soko hili mara moja kwa lengo la kukuza uchumi wa wilaya, mkoa na taifa kwa ujumla," alisema Kamishna Fatma.

Christina Muwakatope, Meneja Biashara na Masoko wa (Kadco), alisema wako tayari kulitangaza soko hilo na kutoa elimu kwa wananchi, abiria na watalii wanaotumia uwanja huo wa ndege ikiwa ni moja ya hatua ya kutangaza utalii na mazuri ya nchi.

"Tutafanya utangazaji wa kutosha, lakini tunaomba mkuu wa wilaya uwatumie watendaji wako wa biashara ngazi ya wilaya na hata wizara kwa ujumla kutangaza soko hilo linalotarajiwa kufunguliwa katika lango la KIA," alisema.

HABARI KITAIFA

# Dalili za matunda mpango wa Tasaf

**Na Elizabeth Zaya**

MPANGO wa kunusuru kaya masikini unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), umeanza kuzaa matunda kwa walengwa katika Halmashauri ya Makambako mkoani Njombe baada ya maisha ya walengwa hao kuanza kuboreka.

Maisha ya walengwa hao yameanza kuboreka kutokana na kuanzishiwa miradi ya ujasiriamali na TASAF ambayo imewawezesha kupata kipato cha kufanyia mambo ya maendeleo ikiwamo kuanzisha vikundi vidogo vidogo vya ujasiriamali.

Nipashe lilitembelea baadhi ya wanufaika wa mpango huo katika Halmashauri ya Makambako na kujionea miradi ya walengwa hao ikiwamo ya ufugaji mbuzi, nguruwe, kuku na kilimo cha mahindi, papai, mahindi na alizeti.

Mbali na miradi hiyo, pia wengi wao walikuwa wamejenga nyumba bora za tofali za kuchoma zilizoezekwa kwa bati, huku wakionyesha nyumba zao ambazo walikuwa wakiishi awali kabla ya kuingizwa katika mpango wa kunusuru kaya maskini.

Walengwa hao waliishukuru serikali kwa kuwakomboa kutoka katika hali duni zaidi kupitia mpango wa TASAF na kuwafungua kiakili kuwaingiza katika shughuli za ujasiliamali kupitia mafunzo ambayo wamekuwa wakiwapatia.

Getrude Mgohirwa, mkazi wa kijiji cha Usetule katika Kata ya Mhongole, alisema tangu mumewe alipofariki dunia miaka 20 iliyopita, alikuwa akiishi maisha magumu na watoto wake sita, ikiwamo kukosa uhakika wa mlo mmoja kwa siku na kukosa uwezo wa kuwanunulia watoto wake sare za shule na mahitaji mengine.

Alisema baada ya kuingizwa katika mpango huo kupitia uongozi wa kijiji, maisha yao yalianza kuboreka na kuanza kuwa na uhakika wa chakula na kumudu kuwahudumia watoto wake ambao walikuwa wanasoma.

"Kwa kweli hatuna cha kusema zaidi ya kuishukuru serikali kupitia TASAF kwa kutuondoa katika hali ile, hakuna mtu mwingine ambaye anaweza kusimulia vizuri zaidi maisha niliyokuwa naishi na watoto wangu baada ya mume wangu kufariki. Ilikuwa inafika mahali ndani kunakuwa hakuna chakula cha kuwapatia watoto," alisema Getrude na kuongeza:

"Hata wale ndugu ambao wakati mwingine walikuwa wanatusaidia ilifika kipindi kama wametuchoka na aibu yenyewe tulikuwa tunaona kuwaomba kila siku, tunaamua kulala na njaa, lakini Mungu ni mkubwa mpango huu ulituokoa, sasa hivi ni watu wengine tofauti."

Alisema sasa wanachakula cha kusaza, watoto wake ambao bado wanasoma anaweza kuwahudumia na hata kuwa na akiba ya kutosha kupitia msaada huo anaopatiwa na TASAF wa fedha na miradi mingine ya ufugaji na kilimo.

"Mume wangu aliniacha katika kanyumba kadogo kamajani na ilikuwa ikifika kipindi cha masika tulikuwa tunanyeshewa na mvua kabisa tukiwa ndani kwa sababu ilikuwa inavuja, lakini sasa hivi hayo maisha tumeshayasahau, kupitia msaada wa TASAF tunaishi katika nyumba bora," alisema Getrude.

# TMEA sasa kuipaisha Tanzania bidhaa kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

UCHUMI wa Tanzania unatarajiwa kupaa kufuatia mapinduzi ya kibiashara kidigitali kuingizwa kwenye biashara za bidhaa za kilimo.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi Mkazi wa TradeMark East Africa, tawi la Tanzania, John Ulanga, wakati akifungua mafunzo ya matumizi ya mfumo mpya wa biashara za bidhaa za kilimo kupitia mtandao wa Agricultural Trade Information System (ATMIS), jijini Dar es Salaam,

Ulanga alisema, Trade Mark East Africa (TMEA), imefanya ujenzi wa mifumo ya kidigitali ya kufanya biashara nchini Tanzania kuongeza ufanisi wa kufanya biashara za kitaifa na kimataifa, kufuatia matumizi ya mifumo ya kidigitali katika kuomba vibali mbalimbali na kulipia kidigitali, kutaongeza kasi ya kufanya biashara kwa wafanyabiashara na kupunguza muda wa kusubiri kupata vibali na kulipia kwa urahisi.

**Tanzania ndio nchi inayoongoza kwa fursa nyingi zaidi za kibiashara katika nchi za Afrika Mashariki, kufuatia kupakana na nchi sita zisizo na bahari.**

Ulanga alisema Tanzania ndio nchi inayoongoza kwa fursa nyingi zaidi za kibiashara katika nchi za Afrika Mashariki, kufuatia kupakana na nchi sita zisizo na bahari. Hata hivyo, ilishindwa kuchangamkia fursa hizo kutokana na kufanya biashara kizamani kwa kutumia njia za kianalojia za kuomba vibali.

Alitaja baadhi kazi za TMEA katika kuboresha mazingira ya biashara Tanzania kuwa ni pamoja na kuziwezesha bidhaa kuyafikia masoko ya Afrika Mashariki kwa kugharimia maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam yaliyogharimu zaidi ya Sh. bilioni 60, ujenzi wa vituo vya pamoja vya forodha (OSBP) na kuboresha mifumo ya Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), vilivyotumia Sh. bilioni 53 na kujenga mfumo wa OSIS unaotumiwa na Wakala wa Barabara nchini (Tanroads), uliogharimu Sh. bilioni mbili.

Aidha, TMEA imetumia Sh. bilioni 2.5 kuboresha na kugharamia mapitio ya Sera ya Biashara, Sera ya Uwekezaji, maandalizi ya Sera ya Ubora, Maandalizi ya Sera ya Kuuza Nje, Mikataba ya WTO. Pia imetumia Sh. bilioni tatu kugharimia kuondolewa kwa vikwazo visivyo vya kikodi, Sh. bilioni 6.5 kwa Shirika la Viwango nchini (TBS), kujenga mifumo ya ubora na Sh. bilioni sita kujenga uwezo wa kidigitali kwa TFDA, MOA, TBS, TMX, TCCIA na ZNCCIA.

Ofisa Mwandamizi toka Wizara ya Kilimo, Mdili Katemani, alisema mfumo wa ATMIS, utawezesha wizara hiyo kutoa vibali kwa kuuza nje mazao na kuingiza nchini kwa njia ya mtandao, vyeti vya ubora wa bidhaa za kilimo, kufanya malipo kwa mtandao, na kupatikana wa taarifa za urari wa kibiashara kwa bidhaa za kilimo.



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya CCECC, wakiweka tuta la kudhibiti mwendo wa magari, katika Barabara ya Sinza - Tandale, eneo la Tandale Magharibi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Mil. 400/- kupanua kituo cha afya

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

KIASI cha Sh. milioni 400, kinatarajia kutumika katika upanuzi wa Kituo cha Afya Kisiju Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani.

Hayo yalisemwa na Mganga Mkuu wa Hospital ya Wilaya ya Mkuranga, Dk Stephen Mwambando, alipotembelea kituo na kujionea ujenzi unavyoendelea.

"Upanuzi huo unatarajia kufika ukingoni, ambapo kutakuwa na ujenzi wa maabara, chumba cha upasuaji mdogo, wodi ya kinamama na nyumba ya mganga mkuu," alisema.

Aliongeza kuwa upanuzi huo umefikia ukingoni ambapo kiasi cha Sh. milioni 400 kitatumika kutoka serikali kuu, hali itakayopunguza utegemezi kwa wagonjwa wanaofuata tiba katika hospitali hiyo.

Dk. Mwanandambo alisema kwenye bajeti hiyo watajenga korido kuunganisha jengo la OPD na maabara, kukarabati ofisi ya waganga pamoja na kununua vitanda na mashuka.

Mkuu wa Kituo hicho, Widman Masika, alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Mshamu Munde, kwa juhudi zake na kufanikisha ujenzi huo kujengwa kwa kiwango cha juu.

Diwani wa Kisiju, Abdul Zombe, aliiomba Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuwaangalia kwa jicho la huruma na kuwapatia gari la wagonjwa sambamba na watumishi wenye ujuzi na weledi (27), hatua itakayofanikisha kuwaokoa wagonjwa mahututi wakiwamo wajawazito na watoto.

Zombe aliwaomba wadau wakiwamo wawekezaji, taasisi na mashirika ndani na nje ya wilaya kukisaidia kituo cha afya kizungushiwe uzio ili kuimarisha usalama sambamba na kuwajengea jengo la kuhifadhia maiti.

HABARI KITAIFA

# Vijiji 600 Igalula sasa kupatiwa mawasiliano

BUNGE limeelezwa kuwa leo serikali itatoa orodha ya vijiji zaidi ya 600 ambavyo vitapelekewa huduma ya mawasiliano.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye (pichani), alitoa ahadi hiyo bungeni jijini Dodoma jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Igalula, Mussa Ntimizi (CCM).

Mbunge huyo alitaka kujua ni lini serikali itapeleka orodha ya vijiji vitakavyopatiwa huduma hiyo ili wabunge washauri maeneo yanayopaswa kuipata.

Katika majibu yake, Nditiye alisema orodha hiyo itatolewa leo kwa wabunge ili wajue vijiji hivyo.

**Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itawapatia wananchi wa Kata ya Mmale mawasiliano kwa kuweka minara ya mawasiliano.**

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji ni lini serikali itawapatia wananchi wa Kata ya Mmale mawasiliano kwa kuweka minara ya mawasiliano.

Naibu Waziri huyo, akijibu swali hilo, alisema katika Wilaya ya Uyui zaidi ya wakazi 66,056 wamefikishiwa huduma za mawasilino katika Kata za Kizengi, Loya, Lutende, Mabama na Miswaki.

Pamoja na mafanikio hayo, Nditiye alisema bado kuna changamoto za upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika Kata ya Mmale.



"Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itaviainisha vijiji vya Kata ya Mmale iliyopo katika Jimbo la Igalula kwa kufanya tathmini ya mahitaji kwa ajili ya kuvifikishia huduma ya mawasiliano,"alisema.

Aliongeza kuwa vijiji hivyo vitajumuishwa katika orodha ya miradi itakayoingia katika zabuni zinazotarajiwa kutangazwa Juni mwaka huu.





Mkurugenzi wa Mipango, Utafiti na Sera wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo(TADB), Dk. Nyankomo Marwa (kulia) akitiliana saini randama ya makubaliano na Katibu Mtendaji wa SAGCOT Kichocheo ,.John Kyaruzi (kushoto) yenye lengo la kuboresha mazingira ya upatikaji wa mikopo yenye tija kwa wakulima, jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kufuta malimbikizo mikopo

SERIKALI imesema inakusudia kuyafuta malimbikizo ya fedha za mikopo ya vijana na wanawake ya miaka ya nyuma iliyotakiwa kutolewa kabla ya mwaka 2016 lakini haikutolewa na halmashauri kwa walengwa.

Hatua hiyo inatokana na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kufuatia malimbikizo hayo kusababisha uwapo wa hoja za ukaguzi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Kusudio hilo lilitangazwa jana bungeni na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(Tamisemi), Mwita Waitara, alipojibu swali la Mbunge wa Lupembe, Joram Hongoli (CCM).

Mbunge huyo alisema madeni ya halmahauri hususani mikopo ya vijana na wanawake ya miaka ya nyuma kabla ya 2016 yamekuwa hayalipiki kutokana na halmashauri nyingi kutokuwa na mapato ya kutosha kuendesha halmashauri hizo hasa miradi ya maendeleo.

"Je, ni kwanini madeni hayo yasifutwe ili kuondoa hoja za ukaguzi kwenye halmashauri hizo? mbunge alihoji.





Habari na Augusta Njoji

Akijibu swali hilo, Waitara alisema kwa sasa, kazi ya uhakiki wa takwimu kubaini kiasi ambacho kimelimbikizwa katika halmashauri zote nchini inaendelea na mara tu itakapokamilika taratibu za kufuta malimbikizo hayo zitafanyika.

Alisema kwa sasa, Ofisi ya Rais, Tamisemi inazisimamia kwa karibu halmashauri ili kuhakikisha zinatoa fedha hizo kwa mujibu wa sheria ambayo inasimamia utoaji mikopo hiyo.

Awali, Waitara alieleza kuwa mamlaka za serikali za mitaa zimekuwa zikitoa fedha za mikopo kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa kuzingatia maelekezo ya serikali.

Alisema katika kipindi chote cha utekelezaji hakukuwa na sheria kwa ajili ya kusimamia utengeji na utoaji mikopo hiyo na kusababisha kuwapo kwa changamoto mbalimbali ikiwamo malimbikizo ya fedha ambazo hazikutolewa kwa walengwa katika kipindi husika na kusababisha hoja za ukaguzi kutoka kwa CAG.

# Aibana serikali tishio ustawi wa Serengeti

MBUNGE wa Viti Maalum, Amina Mollel (CCM), amehoji bungeni hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Tanzania kufuatia tishio la ustawi wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kutokana na Kenya kuwa na mpango wa kujenga mabwawa ya kuzalisha umeme.

Mollel alisema kuna taarifa kuwa Kenya inatarajia kutekeleza mpango huo wa kujenga mabwawa makubwa na kwamba ujenzi huo unatishia ustawi wa uwepo wa Hifadhi ya Taifa Serengeti.

Akimjibu swali hilo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constatine Kanyasu, alisema mwaka 2016 serikali ilipata taarifa ya mpango huo uliopangwa kutekelezwa na Serikali ya Kenya na ilifanya uchunguzi.

"Wizara ilifanya uchunguzi wa madhara yatakayosababishwa na miradi hiyo katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa kukusanya takwimu za mtiririko wa maji na kulinganisha na mahitaji halisi ya miradi tarajiwa," alisema.

Aliongeza kuwa uchunguzi ulibaini utekelezaji wa miradi hiyo ungesababisha athari kubwa kwa ikolojia ya Serengeti kwa kuwa takwimu zilizotumiwa na wataalamu wa Kenya kuhalalisha miradi hiyo hazikuwa sahihi.

"Miongoni mwa athari hizo ni pamoja na kuhatarisha ustawi na maisha ya viumbe hai kutokana na ukosefu wa maji katika Mto Mara wakati wa kiangazi," alisema.

Kanyasu alieleza kuwa matumizi ya Mto Mara yanajadiliwa na Tume ya Kuratibu Bonde la Ziwa Victoria (LVBC) chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Alisema majadiliano mbalimbali kuhusu hatima ya Mto Mara au miradi mbalimbali inayoathiri maji ya mto huo ukiwamo ujenzi wa bwawa la umeme la Ewaso-Ngiro nchini Kenya, yanaendelea pamoja na utekelezaji wa Mpango wa Bonde la Mto Mara uliotiwa saini Septemba 2016.



Mollel



Kanyasu

## Wenye uhitaji maalumu waiomba serikali ajira

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

WAHITIMU wa elimu maalumu kutoka katika Chuo cha Patandi mkoani Arusha, wameiomba serikali kuwapatia ajira katika shule zenye uhitaji wa walimu hao, ili kuendelea kuwasaidia wanafunzi wenye uhitaji.

Akizungumza na Nipashe Mdhibiti Ubora Mkuu wa Shule, Kanda ya Kaskazini Mashariki ambaye pia ni Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Endrew Tamamu, kwenye mahafali ya 23 chuoni hapo, alisema chuo kilianza kutoa elimu maalumu mwaka 1996 na wamefanikiwa kutoa walimu ambao kwa sasa wapo katika shule zenye wanafunzi maalumu.

Alisema kuwa chuo hicho kilianza mwaka 1975, baada ya serikali kubadilisha kutoka shule ya kati ambayo ilianza mwaka 1953, na ilipofika mwaka 1996, serikali iliamua kuhamishia mafunzo hayo chuoni hapo, kutoka katika Chuo cha Ualimu Mkoa wa Tabora.

Hata hivyo, alisema chuo hicho ni pekee nchini, kinachotoa elimu maalumu na kina wataalamu wa kutosha katika nyanja za ufundishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wakiwamo wenye ulemavu, uziwi, vipofu, ulemavu wa akili pamoja na usonji.

Pamoja na mafanikio makubwa waliyonayo, huku akiishukuru serikali kwa kuwapatia fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira rafiki chuoni hapo, alisema wanakabiliwa na upungufu wa vifaa vya kufundishia na kuiomba serikali kutatua changamoto hizo.

Mwanachuo Regina Chuwa, alisema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo katika majukumu ya kikazi ni ukosefu wa vifaa katika shule za wanafunzi maalumu, huku alidai kuwa kuwafundisha watoto viziwi, kunahitaji ufumbuzi mkubwa.

Alisema pia shule hizo ni chache nchini na kuiomba serikali kujenga shule za kutosha na ikiwezekana zifanywe shule za bweni, kutokana na hali ya kiusalama ya wanafunzi hao.

"Shule hizi zingefanywa bweni wengine wanatoka mazingira magumu, wanapokwenda nyumbani na kurudi usalama barabarani sio mzuri, tunaomba serikali ilitizame hili," alisema.

# Watoto 1000 mazingira magumu wanufaika

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

SHIRIKA la Compassion Tanzania, limewezesha kielimu watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi ya 1000 wa Kituo cha huduma ya mtoto Babati kilichopo Kanisa la kinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa kituo hicho, Jonathan Moses Mbesere, wakati akitoa taarifa ya kituo hicho kwenye maadhimisho ya kusherekea miaka 20 ya Compassion International Tanzania, yaliofanyika kwenye kanisa hilo Mjini Babati.

Mbesere alisema tangu kuanzishwa kwa Shirika la Compassion, limekuwa mstari wa mbele kutoa huduma ya huruma kwa miaka 67 iliyopita na watoto wengi wa jamii ya kimaskini wamekuwa wanufaika wakubwa.

Alisema nchi ambazo wanawapa ufadhili watoto wa kundi hilo ni Marekani, Uingereza, Korea, Cuba, Canada na Australia, ambao ndio wana wawezesha watoto hao waliokuwa hawana uhakika wa huduma na kuwawezesha ili wasome vizuri na kufaulu.

**Nchi ambazo wanawapa ufadhili watoto wa kundi hilo ni Marekani, Uingereza, Korea, Cuba, Canada na Australia, ambao ndio wana wawezesha watoto hao waliokuwa hawana uhakika wa huduma na kuwawezesha ili wasome vizuri na kufaulu.**

Mbesere alisema Babati kuna vituo sita ambavyo ni Kanisa la Anglikana Singe, Anglikana Nakwa, Kanisa la KKKT Babati, Kanisa la FPTC Babati, Kanisa la Elimu Pentekoste Babati na Kanisa la Mungu lililopo Babati.

Alisema vituo hivyo vimeanza kuwaandikisha watoto kuanzia mwaka 2001 na kila kituo kiliandikisha watoto 230 kwa kupita mitaani na kuwaona watoto wakicheza na kuwabaini wenye hali ngumu.

"Mfano tulikuwa hatutangazi siku ya kuanza kuandikisha hawa watoto, ili tusije kuandika ambao hawatakiwi, badala yake tulikuwa tunatembea na kukuta watoto wanacheza wakiwa hawana viatu, nguo na tunawaambia watupeleke kwao na tukifika tulikuwa tunakuta mazingira ni magumu, mtu ukiomba maji ya kunywa unapewa kwa kikombe cha chuma au plastiki na tulikaribishwa kukalia vigoda," alisema.

Aidha, alisema watoto waliokuwa na uhitaji walikuwa wanachukuliwa kuanzia miaka mitatu hadi saba na kuwapatia huduma zinazotakiwa shuleni kuanzia chekechea, wanahudumiwa wanapokuwa wanasoma mpaka elimu ya chuo kikuu, lakini mhusika hatakiwi kuzidi miaka 22 kabla hajahitimu elimu ya juu.

Alifafanua kuwa watoto waliofanikiwa kuhitimu shahada ni wanafunzi watano, Stashahada (10), Astashahada (20), kidato cha sita (10), elimu ya kidato cha nne (58) na vyuo vya ufundi walihitimu (105), huku akiwataja walioajiriwa ni watoto 42 na waliojiajiri wapo 142.

Miongoni mwa changamoto ambazo alisema zinakikabili kituo hicho ni pamoja na ushiriki wa baadhi ya vijana, katika programu za kituoni kuwa ndogo kutokana na wazazi kutowahimiza vijana wao na ufinyu wa bajeti kuwahudumia vijana ambao wengi wao wako katika vyuo mbalimbali na hivyo gharama zao kuwa kubwa hasa kwa vituo vyenye umri mkubwa.

Mmoja wa wanufaika wa Compassion International, Anna Jonas, aliambia Nipashe kuwa walimkuta barabarani walipomuandikisha na alikuwa anaishi na mama yake ambaye hakuwa na uwezo na Compassion ndio wamemsomesha kuanzia darasa la kwanza mpaka diploma na sasa wamemwajiri Compassion Kituo cha Msoga kilichopo mkoani Pwani.

Aliwataka watoto ambao wanasaidiwa na shirika hilo, kujituma katika masomo yao na kutokubali kushawishika hasa watoto wa kike ambao wengine wamekuwa wakidanganywa na wanaume na kuwapachika mimba.



Mkuu wa wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga (wa tatu kushoto), akichimba kwa sururu wakati akizindua ujenzi wa jengo jipya la halmashauri ya wilaya hiyo, litakalogharimu Sh. bilioni 4.7, katika Kata ya Dongobesh jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mgogoro wa madiwani, mkurugenzi wamkera RC

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amewataka madiwani na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, kuendelea kushirikiana na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Yefred Myenzi, kwa kuwa serikali haina mpango wa kumhamisha eneo hilo.

Mnyeti aliyasema hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa halmashauri hiyo kuhusu mgogoro kati ya Myenzi na madiwani wa halmashauri hiyo.

Alisema mkurugenzi wa halmashauri hiyo, amesimamia halmashauri hiyo kupiga hatua kubwa kwenye maendeleo na serikali haitamhamisha, hivyo madiwani na watumishi waendelee kushirikiana naye kuwatumikia wananchi.

"Kati ya wilaya ambayo inanipa usingizi mzuri ni Simanjiro, ila nashangazwa sijui upepo gani umewapitia leo madiwani mnamkataa mkurugenzi wenu, kwa hoja ambazo hazina mashiko kwani Myenzi hajafuja fedha zozote," alisema Mnyeti.

Alisema malumbano huwa yanawarudisha nyuma, kwa kuwa badala ya kufanya maendeleo wanabaki kulumbana, jambo ambalo halina tija kwao, wala kwa wananchi wa eneo hilo ambao wengi wao ni wafugaji.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, aliahidi kuwasimamia na kuwaunganisha madiwani na watumishi wa halmashauri hiyo, kwa lengo la kuwatumikia wananchi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Jackson Sipitieck, alisema wataendelea kushirikiana, ili kuhakikisha Simanjiro inazidi kupiga hatua ya maendeleo.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Yefred Myenzi, maarufu kama mashine ya kazi, alisema yeye ataendelea kutekeleza wajibu wake, ili kuhakikisha wananchi wananufaika na miradi ya maendeleo ikiwamo elimu, afya na maji.

Mkazi wa Mji Mdogo wa Orkesumet, Magdalena Kivai, alimpongeza mkuu huyo wa mkoa, kwa kuingilia kati suala hilo na kulimaliza, kwa kuwa wananchi waliona malumbano ya viongozi hao hayatawafikisha mahali pazuri.

# Walalamika kutopewa shamba la L.M Investment

**Na Mary Mosha,** SAME

WENYEVITI wa vijiji vya Ndungu, Msufini na Mpirani wilayani Same, mkoani Kilimanjaro, wamelalamikia uongozi wa wilaya hiyo kushindwa kutekeleza agizo la Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wiliam Lukuvi la kuwapatia eneo la ekari 100 kila kijiji kutoka katika shamba la katani la L.M Investment.

Wakizungumza na Nipashe, wenyeviti hao walisema licha ya kufuatilia suala hilo katika ngazi ya wilaya hakuna jitihada zozote zilizochukuliwa hadi sasa jambo ambalo linawapa mashaka na utendaji wa wilaya hiyo.

Paul Gilbert, Mwenyekiti kutoka Ndungu, alisema licha ya kuwa agizo hilo lilitakiwa kutekelezwa ndani ya siku 60 baada ya kutolewa Oktoba 2018, hakuna lililotekelezeka bila sababu yoyote hadi kufikia siku zaidi ya 150.

Alisema hali hii inaonyesha kuwa wananchi wengi hawawezi kupata haki zao kutokana na watendaji kutupiana mpira licha ya kuwa ni agizo la waziri.

**Tunaendelea na ufuatiliaji kuhakikisha tunamaliza kizungumkuti kilichopo kwa kufuatilia wapi agizo hilo limekwamia.**

"Kucheleweshwa kutekeleza kwa agizo hili kunakwamisha maendeleo, kwa kuwa msimu wa masika unaendelea katika wakati wananchi wamechukua maeneo hayo na kulima ili kujiepusha na baa la njaa katika wilaya hiyo," alisema Juma Hemed, mwakilishi kutoka Kijiji cha Mpirani.

Baada ya kutopata jibu kutoka kwa Mkurugenzi Anna-Claire Shija na Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, katika kutekeleza agizo hilo, Nipashe ilizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, kufahamu nini kinaendelea katika kuhakikisha agizo hilo linatekelezeka, alisema watu hao wawili ndio watekelezaji wa agizo hilo na haoni sababu za kuendelea kurushiana mpira.

"Hili ni suala la kutekeleza agizo la Waziri Lukuvi na si kurushiana mpira... nitalifuatilia kwa ukaribu kujua kwa nini miezi mitano imepita na mwekezaji tayari kalipa, kwanini wananchi hawapati haki yao... hatutakubali serikali ya sasa kupakwa matope kwa watendaji wachache ambao hawatekelezi wajibu wao kwa wakati," alisema Dk. Mghwira.

Kamishna wa ardhi Kanda ya Kaskazini, Leo Komba, alikiri kucheleweshwa kwa utekelezaji wa agizo la waziri Lukuvi kutokana na sababu mbalimbali za kiutendaji kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Same pamoja na Mkurugenzi wa halmashauri hiyo.

"Tunaendelea na ufuatiliaji kuhakikisha tunamaliza kizungumkuti kilichopo kwa kufuatilia wapi agizo hilo limekwamia," alisema.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa shamba hilo, Alan Abas, aliiambia Nipashe kuwa, anasikitika kuwa tayari walishalipia kwa kadri walivyoelekezwa na halmashauri ili shamba hilo liweze kupimwa, lakini badala yake hakuna kinachoendelea.

"Waziri Lukuvi alitoa miezi miwili shamba hilo liweze kupimwa na sisi tuliandikiwa barua ya kututaka tulipie fedha kiasi cha Sh. milioni 4.9 kwa ajili ya upimaji, lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea na kinatuathiri kwa kuwa hakuna uzalishaji unaoendelea, hivyo tunaiomba mamlaka husika kuharakisha upimaji," alisema.




Mwendesha guta akipangua mizigo, baada ya kudondoka katika eneo la Magomeni Mwembechai, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# ATE kutoa tuzo kwa mwajiri bora

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Waajiri Tanzania (ATE), kimezindua rasmi mchakato wa kumtafuta mwajiri bora wa mwaka huu lengo likiwa ni kutambua mchango wa waajiri wenye misingi bora ya usimamizi wa nguvu kazi na rasilimali watu ili kuwawezesha kutimiza wajibu wao kwa ajili ya kuongeza uzalishaji kibiashara.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Dk. Aggrey Mlimuka, alisema tuzo ya mwajiri bora wa mwaka (EYA) ni zoezi lililoanzishwa na kuendeshwa kila mwaka na Chama cha Waajiri Tanzania tangu mwaka 2005.

"Tuzo za mwaka huu zimepanuka sio tu kujali rasilimali watu bali kutambua waajiri wanaofuata taratibu za kitaifa na kimataifa katika uendeshaji wa biashara zao," alisema.

Alisema ushiriki wa tuzo ya mwajiri bora umeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na ukweli kuwa waajiri wengi wamehamasishwa kuthamini watu katika kufanikisha shughuli za biashara kama nyanja muhimu ya usimamizi wa rasilimali watu mahali pa kazi.

Dk. Mlimuka alisema mwaka huu 2019 kutokana na maoni waliyopokea kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, wadau na wataalamu wetu mbalimbali, tuzo ya mwajiri bora kwa mwaka huu wameongeza vipengele vipya vitatu na kufikia vipengele 38 kutoka 35 vilivyokuwapo awali.

Alivitaja vipengele vilivyoongezeka kuwa ni mwajiri bora anayeendeleza mafunzo ya ujuzi wa kazi kwa wahitimu (Internship), Mwajiri bora anayetoa mafunzo ya Uanagenzi na Mwajiri Bora anayezingatia hakirasilimali (local content).

"Lengo la kuongeza vipengele hivi ni kuendelea kuziboresha tuzo hii na kuongeza ushindani miongoni mwa washiriki na pia kujaribu kugusa kila eneo ambalo litaleta tija katika ukuzaji na uendelezaji wa rasilimali watu katika maeneo ya kazi." Dk Mlimuka alisema.

Dk. Mlimuka alisema tuzo hizo mpya zitakuwa ni nyongeza ya zile ambazo zimekuwa zikitolewa katika masuala ya utawala na uongozi, ubora katika usimamizi wa rasilimali watu, bidhaa au huduma, uzalishaji na ubunifu, uwajibikaji katika mwenendo wa biashara, utendaji unaokidhi, ushirikishwaji wa mwajiriwa, ukuzaji wa vipaji, mafunzo na maendeleo pamoja na usalama wa mwajiriwa katika mazingira ya kazi.

# Ukataji miti wahatarisha ukame Same, Mwanga

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

BALOZI wa mazingira nchini Tanzania, Padri Msafiri Aidan, amesema wilaya za Same na Mwanga zina changamoto kubwa ya uharibifu wa mazingira ikiwamo ukataji miti ovyo na uchomaji wa mkaa hali inayochangia kuongezeka kwa ukame kwenye wilaya hizo.

Akizungumza na Nipashe mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro, alisema kuna haja ya serikali kubadilisha sheria ya mazingira kutokana na iliyopo kupitwa na wakati.

Alisema, asilimia 80 ya uoto wa asili umepotea katika wilaya hizo kutokana na miti mingi kukatwa kwa matumizi ya mkaa na kuni.

"Ukiangalia wilaya za Mwanga na Same ndizo zinaongoza kwa tatizo la ukame na hali hiyo inatokana na wakazi wa maeneo hayo kukata miti ovyo, kwa kuwa shughuli yao kubwa ni uchomaji wa mkaa, ambao unasafirishwa katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam," alisema.

Alisema serikali pamoja na wadau mbalimbali wa mazingira wanatakiwa kuwapatia wananchi wa wilaya husika nishati mbadala ili waweze kuachana na shughuli hizo haramu.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, alisema msitu wa Kileo umevamiwa na watu wasiokuwa na moyo wa kizalendo wa kutunza mazingira na kusababisha uharibifu wa mazingira.

"Nimeshuhudia eneo kubwa la hifadhi ya msitu huo, ambao ni sehemu ya chanzo cha maji, likiwa limekatwa miti huku kukiwa na zaidi ya matanuru 12, mengine yakiwa yanafuka moshi na mengine yakiwa kwenye hatua za kuwashwa moto kwa ajili ya kupata mkaa," alisema.

Alisema kuwa kutokana na uharibifu huo, serikali wilayani humo imeshawachukulia hatua za kisheria Mwenyekiti wa Kijiji cha Kileo, Kazeni Mcharo na Mtendaji wa Kijiji hicho, Rista Sumpa, kwa kushindwa kusimamia msitu wa hifadhi wa Kileo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Aprili 30, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 15

**Ukosefu wa ajira unapotetemesha heshima ya taaluma, vyeti, shahada**


Ukurasa 18.

**JE, WAJUA?**

Sokwe mtu wapiga 'selfie' DRC


Ukurasa 17

## Dhahabu barani Afrika yatoroshwa kila mwaka



# Mikakati kuinua ufaulu Mbeya yazaa matunda

Ukurasa 16



Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Naibu Kamishina wa Polisi (DCP), Ahmed Msangi. **PICHA: MTANDAO**

## ELIMU KUTOKA POLISI

# MALEZI BORA NI NJIA YA KUZUIA UHALIFU NCHINI

USALAMA ni dhana ya kuwa huru kutokana na hatari au hofu fulani ndani ya Jamii.

Jukumu la kuimarisha Usalama wa raia na mali zao ni kazi ya msingi ya kikatiba lililopewa Jeshi la Polisi kwa lengo la kuhakikisha wananchi na mali zao wanaishi kwa amani na utulivu.

Ndani ya Jamii kuna mifumo mbalimbali ambayo inatakiwa kufuatwa ili Jamii iweze kuishi katika mazingira ya amani na usalama.

Mifumo hiyo hufanyakazi kwa kutegemeana ambapo mfumo mmoja ukiwa na tatizo unapelekea mfumo mwingine kushindwa kutekeleza majukumu yake kama inavyotarajiwa.

Miongoni mwa mifumo hiyo ndani ya jamii ni mfumo wa malezi ya watoto ambao huanzia ngazi ya familia, mfumo wa dini, mfumo wa kisiasa pamoja na mfumo wa ulinzi na usalama.

Mfumo wa malezi unaohusika na jukumu la malezi ya watoto huanzia ngazi ya familia pale mtoto anapozaliwa mpaka kufikia umri wa kujitegemea.

Ikiwa mtoto hatapata malezi mazuri kupitia mfumo wa malezi na mfumo wa kidini ambao humjenga mtoto kiroho, mtoto huyo hujikuta katika makundi mabaya ndani ya jamii na hivyo kupelekea kutenda vitendo viovu au kwa lugha nyingine uhalifu.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwalea watoto katika malezi bora yenye misingi ya kidini ambayo kwa ujumla hukataza matendo maovu ambayo kwa lugha ya kiusalama huitwa uhalifu, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Naibu Kamishina wa Polisi, (DCP) Ahmed Msangi amewaomba watu wenye mamlaka ya kufanya doria za kiroho ili waweze kushirikiana katika kutokomeza uhalifu hapa nchini.

Doria za kiroho hutekelezwa na viongozi wa dini kwa kufanya mahubiri, kukataza kufanya vitendo vya uhalifu ndani ya jamii kupitia nyumba za ibada na mikutano ya hadhara ili jamii iondokane na uhalifu.

"Viongozi wa dini wana jukumu la kuhakikisha wanafanya mahubiri yanayohamasisha umoja na utengamano ndani ya jamii pamoja na kukataza waumini kuacha kutenda dhambi ambayo kwa lugha ya kiusalama tunaweza kufananisha na uhalifu". DCP Msangi.

Jeshi la Polisi kupitia Kamisheni yake ya Polisi Jamii, liligundua kuwa linatumia nguvu kubwa katika kupambana na wahalifu ambao wamo ndani ya jamii na tunashirikiana nao katika kufanya ibada Kanisani na misikitini hivyo, ushiriki wa viongozi wa dini katika kupambana na uhalifu ni matarajio yetu utabadilisha watu wengi ndani ya jamii na kuwa watu wema.

Pia, amewaomba viongozi wengine wa mikoa kuhuisha na kuanzisha kamati hizo za amani za mikoa ili ziweze kushuka hadi ngazi ya wilaya kwa lengo la kuwa na mkakati wa pamoja katika suala la kubaini viashiria vya uhalifu na wahalifu.

Ushirikiano baina ya Jeshi la Polisi na viongozi wa taasisi za dini kupitia kamati hizo za dini ngazi ya mkoa hadi wilaya itakuwa ni chachu ya mapambano dhidi ya uhalifu na wahalifu katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao ili kujenga jamii yenye hofu ya uhalifu ndani ya jamii.

***Imetolewa na;***
***Kitengo cha Uhusiano***
***Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.***
***S.L.P 9141***
***Dar es Salaam***
***Baruapepe habariphq@yahoo.com, habari.phq@tpf.go.tz*** ***ITAENDELEA***



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Waandishi mnachafua Kiswahili!

NYIE waandishi endeleeni kuchafua lugha yetu ya taifa (Kiswahili), ila mimi sitochoka kuwakumbusha na kuwakosoa kila mnapotumia maneno yanayopotosha Kiswahili.

Kila neno lina kipindi chake. Maana yake kila neno lina wakati wake au kipindi linaposibu au kufaa. Methali hii hutumiwa kumwerevusha mtu anayesema maneno fulani pasipofaa au yasipohitajika. Pia twakumbushwa kuwa kila jambo lina wakati wake; hamna linalofanyika likafana kabla ya wakati wake.

Sikatai kuwa kuna maneno ya kihuni yanayozungumzwa vijiweni na mitaani. Ni watu wachache wanaoelewa maana ya maneno hayo; si wote. Kwa hiyo ni muhimu kutumia maneno halisi ya Kiswahili yanayoeleweka mijini na vijijini. Kwa maana hiyo, ni rahisi wageni wanaojifunza Kiswahili kuelewa matumizi sahihi ya maneno.

"Jeuri ya fedha ... Zahera kuvuta silaha matata" ni kichwa cha habari cha gazeti mahiri la michezo nchini. Maana halisi ya 'silaha' ni kitu chochote kwa mfano rungu, kisu, bunduki n.k. kinachotumiwa kupigana na kujeruhi au kuua; vuruga mipango ya watu, haribu mali ya watu.

'Matata' ni hali ya kugombana inayozuka miongoni mwa watu; ukorofi; mtu mwenye tabia ya ugomvi. Je, ni kweli kuwa Zahera atailetea Yanga 'silaha matata?' Ukurasa wa pili wa gazeti hilo kichwa cha habari kimeandikwa: "ZAHERA SILAHA." Maana ya 'silaha' nimeieleza kwenye paragrafu ya juu. Je, Zahera ni silaha?

Kichwa kingine cha gazeti hilohilo kiliandikwa: "Kumbe Yanga wanataka tu ndoo buana!" Hebu tuone maana ya maneno mawili ya mwisho: 'Ndoo' ni chombo cha bati au plastiki cha kuhifadhia vitu vya majimaji; chombo kidogo kama vile cha buyu kilichofungwa kamba cha kutekea maji katika kisima kirefu. Chombo cha kutilia maji chenye umbo la mche duara ambacho hutengenezwa kwa bati au plastiki na aghalabu huwa na ujazo wa lita 20 au 10.

Sijui siku hizi mafunzo ya uandishi yakoje. Tuliosoma enzi za mkoloni tuliambiwa beleshi/sepetu tuliite hivyo na si 'kijiko kikubwa.' Siku hizi maneno hutumiwa ndivyo sivyo. Kombe ni kitu cha thamani kinachotolewa kuwa kielelezo cha ushindi katika mchezo kama vile mpira wa miguu; kandanda/kabumbu/soka n.k. Pamoja na ukweli huu, waandishi wa michezo hutumia 'ndoo' kuwa m-badala wa kombe!

Aidha 'kombe' ni neno lenye maana zaidi ya hiyo. 1. Sahani kubwa ya kaure (chombo kilichotengenezwa kwa udongo wa aina hiyo); 2. Maakulati maalumu yanayoandaliwa na somo kwa bwana harusi na watu wake wa karibu; chakula kinachopelekwa msikitini kuwa ni sadaka; 3. Dawa ya kunywa inayotokana na maandishi ya Kiarabu; 4. Mmea unaotambaa wenye sumu inayotiwa kwenye ncha za mishale; 5. Sehemu iliyopinda katika nanga au kiopoo.

'Buana' si neno la Kiswahili ila waandishi wa michezo hulazimisha kuwa maana ya bwana kwa sababu wazijuazo wenyewe! Baadhi yao huandika 'bana' badala ya bwana, almuradi wanajiridhisha wenyewe! Kwa kuwa wao ni macho na masikio ya wasomaji, wanapaswa kuandika lugha sahihi inayoeleweka badala ya kupotosha maneno. Bwana si 'bana' wala 'buana.'

"Yaani huyu jamaa alipotea jana, maana kama si Profesa Ndalichako sijui ingekuwaje pale. Waitara mbona ulifanya hivyo mbele ya wageni kutoka Uganda? Dah uwe unajiandaa mtumishi wewe kwani bila kufanya hivyo itakuwa sheeda." Hii ni sehemu ya habari iliyoandikwa na mwandishi anayefuatilia vituko vya ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Dodoma.

'Dah' na 'sheeda' ni lugha ya nchi gani? Mwandishi alitumia neno 'dah' kwa maana ya 'do!' yaani tamko litolewalo kuonesha mshangao au kushtushwa na jambo fulani. Hata hivyo 'sheeda' si neno la Kiswahili ingawa baadhi ya waandishi hulitumia eti kwa maana ya 'shida!' ambalo maana sahihi na halisi ni hali ya kupungukiwa na mahitaji muhimu ya lazima kama chakula, malazi n.k.

Mwandishi huyo alimalizia habari yake hivi: "Chezea watu wa Igunga wewe, usiwe na haraka kujibu kabla ya kujiandaa ujue Dk. Kafumu anatoka koo za kichifu." Neno 'chezea' sasa latumiwa hata kwenye matangazo: "Hapana chezea ... Pesa Up" badala ya "usichezee ... Pesa Up." Waandishi na watangazaji hupotosha maneno ya Kiswahili kila uchao.

"Taarifa za tukio hilo zinaeleza kuwa marehemu alijinyonga kwa kutumia kamba ya katani ambayo aliifunga katika dali ya paa la chumba cha nyumba aliyokuwa akiishi na mumewe katika kijiji cha Majengo mjini Tunduru." Maana ya 'dali' ni kikomo, tama au mwisho kwa lugha ya kishairi. Hapana shaka mwandishi alikusudia neno 'dari' lenye maana mbili: 1. Sehemu ya juu ya nyumba iliyo chini ya paa na 2. Sehemu ya nyuma ya chombo ambayo watu hukaa na chini huwekwa mizigo; sitaha.

"Hii kali! Mwamuzi alewa amwaga kojo uwanjani." Nimeandika mara nyingi kuwa kuna maneno ya kutumia kwenye mazungumzo tu lakini si kuandikwa lakini bado waandishi hawanielewi! 'Kojo'si neno la kuandikwa kwani neno sahihi ni 'mkojo' yaani majimaji yanayotoka mwilini kupitia utupu wa mbele. Uchafu wa majimaji yanayojikusanya katika kibofu na kutoka nnje kwa njia ya tupu ya mbele ya mtu. Kichwa cha habari ya mwandishi kingeandikwa: "Mwamuzi mlevi akojoa uwanjani."

"Tuko kitaani kwa sasa shangwe ni kama lote ..." Hapa msomaji hana anachoelewa kwa sababu sentensi imeandikwa kwa maneno ya kihuni yanayozungumzwa mitaani. Hakuna 'kitaa' bali ni mtaa. Nashindwa kuelewa maana ya "shangwe ni kama lote!"

Methali: Kuchamba kwingi mwisho huondoa mavi.

***marobarnabas@yahoo.com***
***0784/0715 334 096***

UCHAMBUZI

NA MICHAEL ENEZA

# Ukosefu wa ajira unapotetemesha heshima ya taaluma, vyeti, shahada

UMUHIMU wa washikadau katika utoaji wa elimu unafahamika kama sehemu ya mfumo wa elimu kwa jumla, ila umekuwa ukibadilika kulingana na wakati, ikiwa ni pamoja na malengo ya elimu wakati uliopo.

Zipo hatua tatu za kuhusika kwa washikadau ambazo Tanzania imepitia tangu uhuru, na inaelekea sasa kuna kitu kama mparaganyiko katika uhusika huu.

Hata hivyo, huenda ukawa ni chanzo cha kupambanua vyema zaidi malengo ya elimu, ili kuhusika kwa washikadau kusisuguane na mahitaji ya utoaji wa elimu.

Ni suala la kuingia katika mchanganuo wa kina kuhusu elimu yenyewe, wahusika wake na jinsi ya kuipambanua, ili waanze kujipanga upya.

Tatizo ambalo linafikisha sekta ya elimu njia panda ni kutokuwepo kwa uhusiano kati ya uhitimu na kuwa na shughuli ya maisha (occupation) ambalo ni suala tofauti na ajira kama hitaji la kipato kimaisha, kiuchumi.

Suala la shughuli ambayo mtu anakuwa huru kuifanya au anaweza kuifanya mara anapotoka shule au chuo ndiyo inaitwa 'kujiajiri,' lakini mara nyingi hata wenye shahada za juu kitaaluma wamegwaya kupata ajira halisi.

Kupata ajira inayoendana na kiwango cha elimu alichofikia mtu ni tatizo, ingawa bado ndiyo lengo halisi la maisha na elimu kwa jumla, lakini bado ni tatizo la ziada ukilinganisha na suala la kuwapo kwa ajira kama uhakikisho wa maisha.

Tatizo hilo halikuanza juzi, na hadi ilipofikia mahali ambapo hakuna kiwango cha elimu kinachohakikisha ajira kwa mhusika, bado ilikuwa ni suala la ngazi ya kitaaluma, kusoma alikofikia mhusika, na tatizo la ziada ni hili la kuchagua kazi.

Imefika mahali ambapo ngazi zote za elimu zinatoa watu zaidi ya wanaohitajiwa katika soko, na wale wenye elimu zaidi katika tasnia husika huanza kuwasonga wenye elimu duni zaidi, hivyo unasikia kuanzia mwakani wenye shahada za vyuo vikuu watakuwa wanaajiriwa kufundisha shule za msingi.

Vyeti vitakuwa sasa havina thamani, na wenza wake, stashahada nazo zitakuwa ziko ukingoni kukosa umuhimu, shahada zikienea.

Katika kipindi kilichofuata uhuru, ambako tatizo la ajira halikuwapo, mitaala ilikuwa ni kila kitu lakini likaingia tatizo la uwiano kati ya mwelekeo wa taifa na elimu inayotolewa na wengi watasema tatizo la kufundisha na viwango vya walimu na wanafunzi sawia lilianzia hapo.

Hata hivyo, hali halisi ni kuwa kuanzia mwisho wa miaka ya 1960 bei ya mazao muhimu nchini kama pamba, karafuu n.k. ilianza kushuka katika soko la kimataifa huku bidhaa za viwanda zinazoagizwa kutoka nje zikipanda bei.

> Imefika mahali ambapo ngazi zote za elimu zinatoa watu zaidi ya wanaohitajiwa katika soko,..

Mwaka 1985, wakati akiondoka madarakani, Mwalimu alisema mwaka 1965 tulikuwa tunahitaji tani moja ya pamba kununua trekta, lakini mwaka 1985 tunahitaji tani 10 za pamba kununua trekta kama hilo, hoja iliyovuma nchi za Magharibi.

Wanaharakati wakamwita Saint Julius aliyetoa hii 'parable' (mfano) wa tani 10 za pamba na trekta. Kimsingi tulikuwa tunafukarika, siyo kuendelea.

Kipindi cha miaka ya kati 1980 hadi 1990 ilikuwa ya kuanza kwa ujasiriamali wa kipato cha ziada, kwani ajira bado zilikuwa zinapatikana ingawa kuuzwa na kufungwa kwa mashirika ya umma na 'videco' (mashirika ya uchumi ya wilaya na mikoa) kulileta tatizo la ajira mbadala.

Wengi waliopunguzwa hawakupata mahali pengine pa kuajiriwa na wakaanza kufanya biashara za mitaani, na miaka ya 1990 ndipo zoezi la kupunguza wafanyakazi kwa nguvu wakati matumizi ya kompyuta yakianza kuenea kulipotekelezwa.

Kulikuwa pia na msukumo wa kuwa na mishahara inayoendana na ngazi ya kitaaluma, wao huita 'mishahara shindanishi,' ili wataalamu wasikimbie.

Kupanuliwa na idadi ya vyuo na vyuo vikuu hasa kutokana na sera za uliberali zilizoondoa vizuizi kwa watu binafsi kufungua shule au vyuo kuliongeza idadi ya wahitimu.

Pia kuna msukumo wa kijamii wa kupanua nafasi za elimu kwa wahitimu, kuwapo vyuo na hata vyuo vikuu katika kanda na mikoa tofauti kama suala la ustawi wa jamii, huku matumizi ya kompyuta yakipunguza idadi ya watu wanaohitajiwa imekuwa ndiyo hali halisi kwa zaidi ya miaka 10 sasa.

Ikafikia mahali ambapo hakuna tena ajira serikalini, licha ya kuwa ndiyo tegemeo la ajira za kitaaluma kwani kwingine anakuwa ni mwenye mali, vijana wake wasome wasimamie, waajiri 'manamba.'

Ukweli ambao sasa unaanza kujidhihirisha ni kuwa wanaopata shughuli za kufanya katika maisha ni wale wenye mwelekeo wa kiufundi katika eneo hili au lile, iwe ni ufundi wa mashine, umeme, ujenzi, kupaka rangi, na hata udereva wa 'bodaboda' au magari, iwe ni daladala au binafsi, n.k.

Yako maeneo mengine ya ujuzi ambayo si rasmi kwa mfano uimbaji, uzungumzaji (uchekeshaji), na sanaa zinazohitaji mafunzo kama kuigiza, au vipaji kama ilivyo katika uimbaji na kujaribisha vyombo hadi kuvizoea.

Kwingineko taaluma za jadi zinabadilika na kuwa sanaa, kwa mfano uandishi wa habari una maeneo tanzu mapya, hasa uzungumzaji katika vituo vya redio na televisheni; uendeshaji wa sherehe unakuwa mbadala wa 'public relations,' mahusiano ya kitaasisi, kijamii.

Wanaharakati wa kupinga utandawazi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wangeweza kusema kuna hali ya udunishaji wa taaluma na 'urahisishaji' wa elimu kwa jumla, kuwa kinachotakiwa ni kipaji au mafunzo katika eneo fulani uweze kuingia, siyo vyeti au ngazi ya kusoma.

Labda tu kitakachowezesha jamii ithamini elimu na vyeti hapo mbeleni ni kupanuka kwa huduma za kawaida kama ualimu, uuguzi, usalama wa raia (polisi, ulinzi kupitia asasi binafsi au katika serikali za mitaa) ambazo, kama ilivyo michezo, uwezo wa dansi (kunengua) na hata kazi zinazoonekana ni rasmi kama uhudumu wa bar hazina mishahara kamili. Ni malipo ya kujikimu tu.

Katika mifumo iliyoendelea ya kisiasa nchi za Magharibi, siasa inakuwa ni eneo mojawapo la ajira pana nchini, kwani kila chama kinachoshiriki uchaguzi kinahitaji watu wanaogombea kupitia chama hicho, wenye uwezo wa kufafanua hisia zake, zieleweke na zipigiwe kura na wananchi.

Ni katika hali hiyo ambako kazi za ushauri kwa mfano kuandika hotuba kwa mlengo wa aina maalum unaoelekea kundi pana la watu bila kuwasahau wengine wanaounga mkono sera au hisia za chama hicho bila kuwa wakereketwa zinaanza kupata soko.

Ni mazingira ya urahisi wa bidhaa na uwezo wa wagombea kuajiri watu wa muda mfupi, kama vile nyumba au mitaa inakuwa na uwezo wa kuajiri walimu kuwafundisha watoto wao karibu na nyumbani au vituo vya masomo ya ziada vingi tu.

Sasa hivi tatizo linaonekana kama ni la kuwapo kwa shahada na vyeti vya kawaida ambavyo havitoi ajira, tofauti na stadi za maisha (ufundi) ambazo zina uhakika zaidi wa ajira, lakini katika hali halisi tatizo ni uwezo wa kununua na hivyo hitaji halisi la bidhaa.

Kila aina ya taaluma ni bidhaa na maeneo mengi yanahitaji kuwa na msingi wa kutosha wa elimu kwa ngazi ya shahada au ya pili, ili kuingia 'kichwa kichwa' kwa mfano katika eneo la ushauri wa kisiasa, kuandika hotuba, n.k.

Kimsingi uwezo huo wa kuhitaji bidhaa na kuzinunua (ambayo ni pamoja na kuhitaji uwezo kitaaluma na kuutumia kwa mahitaji tofauti ya kijamii, kisiasa au kiuchumi) hali ya kukosekana ajira itapungua lakini haitaisha, kama inavyoonekana nchi zilizoendelea.

Kubadilika mitambo na kutumia ile ya kujisogeza yenyewe na kuhitaji watu wachache, halafu kompuyta zinawezesha mtu mmoja kufanya vitu vingi kwa siku moja tofauti na awali; kujishikiza hapa na pale kitaaluma ndiyo mustakabali wa elimu kwa sasa.



Baadhi ya wahitimu wa mojawapo ya vyuo vikuu nchini. **PICHA: MTANDAO**.

ELIMU

NA NEBART MSOKWA, MBEYA

# Mikakati kuinua ufaulu Mbeya yazaa matunda

## • Kutoka nafasi ya 23 mwaka 2015 hadi ya pili kitaifa mwaka jana

KWA muda mrefu sasa kumekuwapo na ushindani mkubwa katika sekta ya elimu nchini kati ya mkoa mmoja na mwingine ambapo kipimo cha ushindani huo kikiwa ni nafasi ambayo mkoa unashika kwenye mitihani ya kitaifa.

Katika ushindani huo historia inaonyesha kuwa miaka ya 1990, Mkoa wa Mbeya ulikuwa miongoni mwa mikoa iliyokuwa inafanya vizuri kwa kushika nafasi za juu kitaifa kwenye mitihani ya ngazi mbalimbali.

Hata hivyo, hali hiyo ilianza kubadilika miaka ya 2000 pale mkoa huo ulipoanza kuporomoka.

Ulionekana kuporomoka zaidi katika matokeo ya kidato cha nne ya mwaka 2015 uliposhika nafasi ya 23 kati ya mikoa 30, hali ambayo iliwashtua viongozi na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu mkoani humo.

Kufuatia hali hiyo, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Amos Makalla, alilazimika kuwaita wadau mbalimbali wa elimu kwa ajili ya kubainisha eneo lililokuwa linateleza na kuweka mikakati kabambe kwa ajili ya kurejesha heshima yake.

Kikao hicho kilichowahusisha pia walimu wakuu, wakuu wa shule pamoja na maofisa elimu wa kata na wilaya zote, kilipitisha maazimio mbalimbali likiwemo la kuwapatia motisha walimu ambao wanafunzi watafanya vizuri masomo yao kwenye mitihani ya kitaifa.

Aidha, wadau walikubaliana kuwapatia motisha wanafunzi watakaofanya vizuri kwenye mitihani ya kitaifa ya darasa la nne, darasa la saba, Kidato cha pili na cha nne.

Mbali na motisha, walikubaliana pia kuhakikisha miundombinu ya elimu inaimarishwa ikiwamo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ili kuondoa msongamano wa wanafunzi kwenye madarasa pamoja na kuboresha miundombinu ya vyoo.

Katika mlolongo huo, ilianzishwa siku ya elimu ambayo huwakutanisha wadau wote kila mwaka, kwa ajili ya kufanya tathmini ya hali ya elimu kwa mwaka uliopita na kupanga mipango mipya ya mwaka unaofuata.

### KUPANDA KWA UFAULU

Utekelezaji wa maazimio hayo pamoja na mengine ulianza mara moja mwaka 2016.

Hali hiyo imesababisha mabadiliko ya ufaulu ambapo sasa umeanza kupanda hasa kwa wanafunzi wa kidato cha nne na darasa la saba.



Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Paulina Ndigeza (Kushoto), akiwahutubia wadau mbalimbali wa elimu mkoani Mbeya, Machi 21 mwaka huu, wakati wa Kongamano la Elimu.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika (Kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Steven Katemba (kulia), wakipokea Ngao ya Ushindi wa taaluma kimkoa kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila.

> Kile chakula ambacho mtoto hutunziwa awapo shuleni, basi sasa inabidi akipate hukohuko shuleni…ni lazima wote tushirikiane kwa mfumo tutakaoona unafaa, ila watoto wale chakula shuleni,



Mmoja wa wanafunzi wa kike waliofanya vizuri kwenye mitihani ya kidato cha pili mkoani Mbeya, akipokea zawadi kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati wa Kongamano la Elimu lililofanyika Machi 21, jijini Mbeya. **PICHA ZOTE: NEBART MSOKWA.**

Katika matokeo ya Kidato cha nne ya mwaka 2016, Mkoa wa Mbeya ulipanda kutoka nafasi ya 23 ulioshika mwaka 2015 mpaka nafasi ya 13 ambapo kwa mara ya kwanza zawadi zilitolewa kwa walimu, wanafunzi na shule zilizofanya vizuri.

Matokeo ya Mwaka 2017, mkoa ukapanda tena kwa kasi kutoka nafasi ya 13 mpaka ya sita, zawadi zikatolewa tena na mipango mipya ikaandaliwa.

Matunda ya ushirikiano wa wadau katika kuimarisha ufaulu yalionekana zaidi katika matokeo ya kidato cha nne ya mwaka jana (2018) ambapo Mkoa wa Mbeya ulishika nafasi ya pili kitaifa.

Mbali na ufaulu wa kidato cha nne kupaa, ufaulu katika mitihani ya darasa la saba nao umekuwa ukipanda kila mwaka ambapo mwaka 2016 ulikua kwa asilimia 60 na mwaka 2017 ukapanda hadi kufikia asilimia 67 na mwaka jana ukafikia asilimia 75.

Mwezi Julai Mwaka 2018, Rais John Magufuli alifanya mabadiliko ya wakuu wa mikoa.

Alimhamisha aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Amos Makala na kumpeleka Katavi, huku akimteua Albert Chalamila kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya.

Pamoja na mengine, Makalla alimkabidhi Chalamila nyaraka zenye mikakati ya kuinua ufaulu wa wanafunzi na akamshauri aendeleze mchakamchaka huo.

### CHALAMILA MSIMAMO ULE ULE

Chalamila na wasaidizi wake pamoja na wadau wa elimu mkoani humo, wameendeleza mipango ya ushindi na kwa mara ya kwanza Chalamila aliongoza kikao cha tathmini kilichofanyika Machi 21 mwaka huu.

Katika kikao hicho zawadi mbalimbali zilitolewa kwa walimu, wanafunzi, shule zilizofanya vizuri pamoja na wadau waliochangia kuimarisha sekta ya elimu na hivyo kuung'arisha Mkoa huo.

Aidha, kikao hicho kilitumika kupanga mikakati mipya itakayosaidia kuimarisha zaidi sekta hiyo.

Moja kati ya mikakati mipya ni ya utaratibu wa wanafunzi kula chakula cha mchana shuleni.

Chalamila anasema wazazi kwa kushirikiana na wadau wachangie chakula kwa watoto wao wawapo shuleni, hali itakayowafanya wawe na fursa nzuri ya kuelewa wanachofundishwa.

"Kile chakula ambacho mtoto hutunziwa awapo shuleni, basi sasa inabidi akipate hukohuko shuleni... ni lazima wote tushirikiane kwa mfumo tutakaoona unafaa, ila watoto wale chakula shuleni," anabainisha.

### MIUNDOMBINU

Kipaumbele cha pili mkoa ulichojiwekea ni kuhakikisha miundombinu ya shule hasa vyumba vya madarasa, vyoo na maabara vinakuwa katika hali nzuri ambayo itawafanya wanafunzi wasome na kufaulu vizuri.

Chalamila anasema katika Mkoa huo wapo wadau ambao wameiunga mkono Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuchangia ujenzi wa miundombinu hiyo akiwemo mdau wa maendeleo, Ndele Mwaselela ambaye amejenga vyumba vya madarasa katika Kata ya Iyela jijini Mbeya.

Wadau wengine ni pamoja na Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, ambaye amekuwa akisaidia ujenzi wa miundombinu hasa vyoo kwenye shule za msingi na Sekondari mkoani humo.

Anawataka wadau wengine kuendelea kujitokeza kuunga mkono juhudi za serikali ili miundombinu iwe rafiki kwa wanafunzi wa ngazi zote na hivyo kuimarisha sekta hiyo.

"Rais ametoa zaidi ya Sh. Bilioni 29 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu yetu na mkoa wetu ulipata mgawo wa Sh. bilioni 2.3 na tulizigawa katika halmashauri zote na nawashukuru wakurugenzi mmezisimamia vizuri," anasema Chalamila.

### WACHELEWA KUANZA SHULE

Chalamila anasema mwaka huu zaidi ya wanafunzi 6000 wa kidato cha kwanza walichelewa kuanza masomo kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa 143 lakini mpaka kufikia mwanzoni mwa mwezi Machi wanafunzi wote walianza masomo baada ya vyumba hivyo kukamilika.

Anasema vyumba hivyo vilijengwa kwa ushirikiano kati ya serikali, wazazi na walezi pamoja na wadau wa elimu waliotoa michango ya hali na mali.

### KUIMARISHA KKK

Chalamila anasema serikali na wadau mkoani Mbeya, wamekubaliana kuimarisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa watoto wa darasa la kwanza na la awali.

Anasema stadi hizo ni muhimu kwa ajili ya kuandaa msingi mzuri wa wanafunzi ili wakifika madarasa ya juu wawe na uwezo wa kufanya vizuri.

Mbali na kuimarisha KKK, Chalamila anasema pia walikubaliana kuhakikisha uandikishaji wa watoto wa madarasa ya awali na darasa la kwanza unafikia asilimia 100.

Anasema wamekubaliana kuhamasisha wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao shuleni ili kufikia kiwango cha uandikishaji kinachotakiwa.

"Serikali sasa inatekeleza sera ya elimu bila malipo, hakuna mtu atakayekuwa na kisingizio cha gharama... ili tuendelee kufanikiwa ni lazima uandikishaji wa watoto uanzie asilimia 100 na kuendelea," anasema.

### OFISA ELIMU

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Paulina Ndigeza, anawapongeza wadau wote wa Mkoa wa Mbeya kwa ushirikiano katika kuhakikisha sekta ya elimu inapaa kwa kazi.

Anasema mafanikio hayo yametokana na ushirikiano mzuri kati ya serikali, walimu, wazazi na walezi pamoja na wadau ambao wanashiriki shughuli mbalimbali za kielimu.

**INAENDELEA UK.18**

JIELIMISHE

# Dhahabu barani Afrika yatoroshwa kila mwaka

MADINI ya dhahabu yenye thamani ya mabilioni ya dola yanatoroshwa kutoka Afrika kila mwaka kupitia nchi za Mashariki ya Kati na kuuzwa kwenye masoko ya Ulaya na Marekani.

Kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa na shirika la habari la Reuters, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), uliingiza katika nchi zao dhahabu yenye thamani ya dola bilioni 15.1 kutoka Afrika mnamo mwaka 2016 pekee.

Kulingana na uchunguzi wa shirika hilo la Reuters, kuanzia mwaka 2006 hadi mwaka 2016 nchi hiyo ya kiarabu iliingiza tani 446 za dhahabu kutoka nchi za Afrika.

Kiwango kikubwa cha dhahabu hiyo hakikuorodheshwa katika bidhaa zinazouzwa nje na nchi za Afrika.

Wataalamu waliohojiwa na shirika hilo wamesema kiasi kikubwa cha madini hayo kinatolewa nje ya Afrika bila ya kutozwa kodi na nchi zinazozalisha madini hayo hazipati kitu.

Kampuni za madini barani Afrika zimeliambia shirika la Reuters kuwa kampuni hizo haziuzi dhahabu kwa Umoja wa Falme za kiarabu.

Tamko hilo linathibitisha kwamba dhahabu hiyo inaingia katika nchi hiyo kwa njia ambayo si rasmi.

Serikali za Ghana, Tanzania na Zambia zimelalamika kwamba dhahabu ya nchi hizo inatoroshwa kwa kiwango kikubwa na magenge ya wahalifu na aghalabu katika muktadha wa madhara makubwa kwa mazingira na afya ya binadamu.



Wachimbaji wadogo wa dhahabu wakiwa kazini nchini Tanzania. . **PICHA: MTANDAO**

Shughuli za kuchimba dhahabu ambazo hapo awali zilikuwa zinafanywa na wafanyabiashara wadogo katika nchi hizo za Afrika, sasa zimechukuliwa na kampuni kubwa kutoka nje ya Afrika.

Hayo alisema hivi karibuni Rais wa Ghana, Nana Akufo.

Mfano, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ni mzalishaji mkubwa wa dhahabu, lakini nchi hiyo inaambulia kiasi kidogo cha fedha zinazotokana na mauzo ya bidhaa hiyo nje ya nchi.

Dhahabu ya nchi hiyo inaporwa na watu kutoka nchi jirani.

Taarifa ya UN inaonyesha kwamba kituo kikuu ambapo dhahabu ya Afrika inateremshwa ni UAE.

Hata hivyo, mnamo mwaka 2015, China iliingiza nchini mwake, kiwango kikubwa cha dhahabu kutoka Afrika kuliko nchi hiyo ya kiarabu.

Na mwaka 2016 nchi hiyo ya kiarabu, iliingiza dhahabu kutoka Afrika yenye thamani ya dola bilioni 7.4.

Mshauri mwandamizi wa maendeleo ya viwanda wa Umoja wa Afrika (AU), Frank Mugyenyia, anasema kiwango kikubwa cha dhahabu kinauzwa nje ya Afrika bila ya daftari.

Mahitaji makubwa ya dhahabu katika kipindi cha mwongo uliopita pia yameongeza madhara katika mazingira.

Vifaa vinavyotumiwa na wachimbaji wa dhahabu vinaongeza uzalishaji, lakini katika mchakato wa kuchimba dhahabu hiyo, maji ya sumu yanaingia kwenye mito na kuathiri afya za watu wanaotumia maji hayo.

Maji hayo ya sumu yanasababisha maradhi kwenye ini, mafigo, bandama na mapafu.

Serikali za Afrika zinajaribu kutafuta njia ya kuisimamia sekta hiyo kwa sababu inawaingizia wananchi wengi mapato.

Nchini Tanzania, taarifa ya Bunge inaonyesha kwamba asilimia 90 ya dhahabu inayozalishwa nje ya taratibu rasmi, inatoroshwa nje ya nchi.

Sasa serikali inaitaka Benki Kuu ya Nchi hiyo (BoT), inunue dhahabu kutoka kwa wachimbaji.

Serikali ya Tanzania inapanga kuanzisha vituo rasmi vya biashara ya dhahabu.

Bei ya dhahabu sasa inafikia dola 40,000 kwa kilo. Kadri inavyotoroshwa na kuuzwa nje, nchi za Afrika zinaingia hasara ya mabilioni kila mwaka, kwa mujibu wa uchunguzi wa shirika la Reuters. DW



Baadhi ya wadau wa elimu mkoani Mbeya, wakifuatilia hotuba za viongozi mbalimbali wa mkoa huo wakati wa Kongamano la Elimu, Machi 21, mwaka huu.

# Mikakati kuinua ufaulu Mbeya yazaa matu

INATOKA UK.16

Paulina anabainisha kuwa mbali na Mkoa kushika nafasi ya pili kitaifa katika matokeo ya Kidato cha nne ya mwaka 2018, pia shule ya kwanza kitaifa ambayo ni St. Francis ipo mkoani humo hivyo nayo imechangia kuupaisha mkoa huo.

Aidha anasema, mwanafunzi bora kitaifa katika mtihani huo Hope Mwaibanje, pia anatokea mkoani Mbeya na kwamba alisoma shule ya Msingi Lyoto ambayo ni ya Serikali.

"Lakini tulifanya pia mashindano ya Sayansi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) kwa shule za Sekondari ambapo Msichana wa kwanza kitaifa ametoka Mkoani kwetu tena shule ya Serikali ya Lyoto," anasema.

Anatamba kuwa kutokana na mipango iliyowekwa na wadau, Mkoa huo utaendelea kufanya vizuri, lengo likiwa ni kuhakikisha unakuwa wa kwanza kwenye mitihani ya ngazi zote za kitaifa.

WADAU

Mdau wa maendeleo Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela anawashauri wananchi kushiriki katika kuboresha miundombinu ya shule bila kujali tofauti ya itikadi zao za kisiasa.

Anasema Serikali ya Awamu ya Tano ilipotangaza kuanza kutekeleza sera ya elimu bila malipo, baadhi ya wazazi waliamini kuwa kila kitu kitakuwa kinatolewa na serikali, kitu ambacho si kweli.

Mwaselela anasema wazazi, walezi na

JE, WAJUA?

## Sokwe mtu wapiga 'selfie' DRC



Hawavumi lakini wamo! Sokwe wakipiga 'selfie'. **PICHA: MTANDAO**

SOKWE mtu wawili wameshangaza wengi kwa kuweza kuiga mkao wa binadamu waliponaswa kwenye picha iliyopigwa kwa kutumia kamera ya mbele ya simu ya mkononi, maarufu kwa lugha ya mtandaoni kama selfie.

Sokwe hao wamepiga selfie hiyo na askari wa wanyamapori ambao waliwaokoa kutoka kwenye makucha ya majangili walipokuwa wadogo.

Picha hiyo imepigwa katika makao ya sokwe yatima kwenye Hifadhi ya Taifa ya Virunga nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ambapo sokwe hao wamekuwa wakilelewa toka wazazi wao kuuawa na majangili.

Naibu mkurugenzi wa hifadhi hiyo Innocent Mburanumwe, ameiambia BBC kuwa, sokwe hao walijifunza kuiga tabia za binadamu wanaowatunza toka walipokuwa wadogo.

Sokwe hao, kwa mujibu wa Mburanumwe wanadhani askari hao ni wazazi wao.

Mburanumwe pia ameiambia BBC kuwa mama wa sokwe hao waliuawa Julai 2017.

Sokwe hao waliokolewa wakiwa na umri kati ya miezi miwili na minne.

Muda mfupi baada ya wazazi wao kuuawa, sokwe hao waliokolewa na askari na kutunzwa kwenye makazi maalumu ndani ya hifadhi ya Virunga mpaka hii leo.

Kwa kuwa wamekua wakiwa na askari waliowaokoa, Mburanumwe anasema, wanaigiza tabia za binadamu na wanasimama kwa miguu miwili ndio namna yao na kwamba ndiyo namna yao ya kujifunza kuwa binadamu.

"Hata hivyo, haitokei kila wakati," anasema Mburanumwe na kuongeza: "Nilipigwa na mshangao nilipoiona picha hiyo kwani ni picha ichekeshayo... ni jambo la kushangaza kuona namna gani sokwe wanaweza kumuiga mwanadamu na kusimama."

Mburanumwe anasema, kuwa askari wa wanyama pori kwenye eneo hilo hata hivyo si kazi nyepesi au ya raha tele, bali ni kazi ngumu sana.

Askari wanyamapori watano waliuawa mwaka jana na watu wanaodhaniwa kuwa waasi katika shambulio la kushtukiza kwenye hifadhi ya Virunga.

Kwa ujumla, kutoka mwaka 1996, askari wanyamapori 130 wameuawa katika hifadhi hiyo.

Hifadhi ya Virunga ipo Mashariki mwa DRC, eneo ambalo limetawaliwa na vita baina ya serikali na makundi kadhaa ya waasi.

Baadhi ya makundi hayo yamekita kambi ndani ya hifadhi hiyo, na yamekuwa wakishiriki biashara haramu ya ujangili.

BBC

## Vimbunga vinavyopewa majina popote duniani

PENGINE umewahi kusikia vimbunga vikiwa na majina ya kushangaza!

Kipo kinachoitwa Idai kilichosababisha uharibifu mkubwa katika baadhi ya maeneo ya nchi za Msumbiji, Malawi na Zimbabwe Machi mwaka huu.

Hiyo ni katika kile ambacho Umoja wa Mataifa (UN) unasema huenda ni janga baya zaidi la hali ya hewa kuwahi kushuhudiwa Kusini mwa Afrika.

Kuna kimbunga Matthew ambacho kilikumba maeneo ya Haiti, Jamaica, Jamhuri ya Dominika, Bahamas na baadhi ya majimbo ya Marekani, Oktoba mwaka 2016.

Kabla yake, yaani mwezi Septemba mwaka huo, kulikuwa na kimbunga kingine kilichojulikana kama Hermine kilichosababisha uharibifu mkubwa katika Jimbo la Florida, nchini Marekani.

Hata hivyo, kinachokumbukwa zaidi ni kile kinachojulikana kwa jina la Katrina ambacho kiliathiri sana majimbo ya Louisiana, Mississippi na Alabama nchini Marekani.

Pengine swali ni je, vimbunga hivi hupewa vipi majina?

Jibu ni kwamba, vimbunga katika maeneo ya bahari ya Atlantiki, maeneo ya Caribbean na Ghuba ya Mexico hupewa majina na Shirika la Utabiri wa Hali ya Hewa Duniani (WMO) ambalo lina makao yake makuu nchini Uswizi.

Zamani, ni majina ya kike pekee yaliyotumiwa lakini kuanzia mwaka 1979, majina ya kiume yalianza kutumiwa vilevile.

Huwa kuna makundi sita ya majina ambayo hutumiwa kwa mzunguko.

Hii ina maana kwamba majina yaliyotumiwa kwenye vimbunga mwaka huu hayatatumiwa tena hadi 2022.

Majina kwenye orodha hii yanaweza kubadilishwa na WMO.

Orodha hii ilianza kutumiwa mwaka 1979. Kabla ya hapo, jina la kimbunga Fern lilibadilishwa mwaka 1966 na badala yake kukatumiwa jina Frieda. Hakuna sababu iliyotolewa.

**SABABU ZA KUACHA KUTUMIA MAJINA**

Baadhi ya majina huacha kutumiwa hasa kunapotokea uharibifu mkubwa au hasara kubwa, kwamba kutumia tena jina hilo kutafufua kumbukumbu zenye uchungu.

Mfano ni kimbunga Katrina kilichoua watu 2,000 mwaka 2005 na kusababisha uharibifu mkubwa Marekani.

Kimbunga hicho kiliwaacha watu milioni moja bila makao. Mji wa New Orleans, Louisiana uliathirika sana.

Katika WMO kuna kundi la wataalamu liitwalo Kamati ya Vimbunga vya Tropiki ambalo hukutana kila mwaka.

Kundi hilo ndilo huamua ni majina yapi yatatumika tena na ni yapi yataacha kutumiwa.



Moja ya madhara ya vimbunga. **PICHA: MTANDAO**

nda

wadau wanatakiwa kushiriki katika kuboresha miundombinu ya elimu kwa kufuata taratibu kama serikali ilivyoelekeza.

"Serikali inatoa zaidi ya Sh. bilioni 23 kila mwezi kwa ajili ya kutekeleza sera ya elimu bila malipo...baada ya serikali kukataza michango shuleni, kuna watu wanaamini kuwa hawatakiwi kufanya chochote kitu ambacho si kweli, ni lazima tushiriki katika ujenzi wa miundombinu," anasema.

'MAFATAKI'

Mwenyekiti wa machifu wa Jiji la Mbeya, Rocket Mwashinga, anasema viongozi wa mila watashirikiana na Serikali kuwadhibiti wanaume wanaowapachika mimba wanafunzi na kukatisha ndoto zao za maisha.

Chifu Mwashinga anasema kuwa kwa kutumia mbinu zao za jadi watazihamisha mimba kutoka kwa wanafunzi kwenda kwa wanaume wanaowapa mimba wanafunzi ili kukomesha vitendo hivyo.

Anasema ili kukomesha vitendo hivyo kunahitajika ushirikiano wa wazazi, walimu, Serikali na viongozi wa mila na kwamba wao kwa mujibu wa taratibu zao za kimila hawatakiwi kumpeleka mtu mahakamani na badala yake wanamshughulikia kwa kutumia taratibu zao.

"Tunachoomba ni ushirikiano kutoka kwa walimu ili mwanafunzi akipata mimba tumbane amtaje mwanamume aliyempa mimba hiyo... akishamtaja tunamwita, tunamhoji... akikataa sisi tunamhamishia mimba na ataenda mwenyewe kujifungua META (Hospitali ya Rufaa ya Uzazi jijini Mbeya)," anasema.

Aidha anasema, watatumia mbinu zao kulinda maeneo yote ya shule kudhibiti wachawi wanaowasumbua walimu na wanafunzi kwa kuwasababishia magonjwa ya ajabu ajabu, likiwemo la kuanguka ambayo yamekuwa yakisumbua shule nyingi.

ELIMU

## UCHAMBUZI WA KITABU;

# LIGHT ON LIFE's DIFFICULTIES by James Allen

## (Mwanga katika magumu ya maisha)

MAGUMU yanapokuja katika maisha ya mtu hufanana na kikwazo cha mwanga katika chumba chenye giza.

Ndani ya chumba chenye giza ni rahisi kuanguka, kutoona pa kuelekea mpaka pale mwanga utakapoweza kukijaza hicho chumba.

Mwanga hufanya mambo yawe wazi na njia ya kutoka iweze kupatikana.

James Allen ni mmoja ya waandishi ambao kupitia ukumbusho wa maandiko yao wameendelea kuishi hadi hivi leo. Karibu vitabu 18 vimeandikwa na yeye vikiwa na lengo kubwa la kumuibua mtu kujifahamu uwezo wake mkubwa uliomo ndani yake wa kukabiliana na maisha na lolote liwezalo kumtokea.

Kwanza kabisa maisha yetu yalivyo ni matokeo ya mawazo yetu wenyewe yakiambatana na matendo yetu.

Ni vile hali zetu za fikra hutuumbia tujione na furaha au huzuni katika tunayopitia katika maisha ambayo kwa asilimia kubwa ni sisi wenyewe tumechagua kuyapa tafsiri ya kufikiri kwetu.

Hivyo njia ya furaha na mateso ni vile mtu mwenyewe atakavyoweza kuruhusu kufikiri na kutenda.

Mateso ambayo yanatokea katika maisha yetu ni vile tunavyokaribisha mawazo hasi na hisia hasi kunakoshawishi kuchukua hatua ambazo zinazidi kutuumiza na kutukaribishia mateso zaidi.

Binadamu hawezi kujikimbia wala kuikimbia akili yake au mwili wake mwenyewe.

Hivyo, kwa kila jambo atakaloruhusu kupita katika akili basi mwili utaathirika iwe kwa hasi au chanya.

Kuishi anakosemea mwandishi ni kufikiri kwa usahihi na kutenda kwa usahihi. Kwenda kinyume na hili ndipo ambapo maisha huonekana kuwa mabaya na magumu.

Vile uwezavyo kumwona mtu ni jinsi alivyo katika fikra. Hivyo unaweza kusema mtu ni fikra. Na hili halipingani kuwa kila kimtokeacho mtu basi kimeongozwa na sheria ya asili ya kupanda na kuvuna au kisababishi na athari (Law of Cause and Effect).

Hivyo, mtu asione maajabu yoyote katika yale yamtokeayo, asisahau kuwa yeye anaweza kuwa kisababishi cha matokeo anayoyaona kwa chochote.



Wanariadha waliofanikiwa ni wale ambao huona mwanga na kufanya kazi ya kuufikia wakipitia magumu mbalimbali. **PICHA: MTANDAO**

James Allen ni mmoja ya waandishi ambao kupitia ukumbusho wa maandiko yao wameendelea kuishi hadi hivi leo. Karibu vitabu 18 vimeandikwa na yeye vikiwa na lengo kubwa la kumuibua mtu kujifahamu uwezo wake ...

Kuna nukuu isemayo kuwa kwa kila kitu utakacho, kuna gharama ya kulipia. Ukija katika ngazi ya juu ya mtu kama kiumbe wa kiroho pia kuna gharama au thamani ya kuonyesha tabia za kiroho ambazo fedha haziwezi kununua.

Matendo ya huruma, upendo, hekima na furaha hubadilishwa na wengine kwa kutoa na kuishi katika tabia hizi.

Kadri mtu anavyoweza kukua na kuwa nazo hizi tabia, ndivyo anavyoweza kuona mwanga kwa kila tatizo au gumu atakalolipata.

Kukubaliana na asili inavyofanya kazi ni kujiondosha katika mateso na huzuni pale ambapo utaingia katika magonjwa, magumu, maumivu na hata kupoteza watu wa karibu (kifo).

Kwa kuwa huwezi kuzuia asili kufanya vitu kukua, kuchoka na kufa.

Kadri mtu anavyokubali ukweli huu wa kuwa mtu hana kinga dhidi ya kushambuliwa na hali za ugonjwa, kuzeeka na kufa, basi atakavyopitia au kuwaona wengine wakipitia atakubaliana na asili kuwa ni moja ya kitu kilicho nje ya uwezo wake.

Kujitoa kunaumiza maana ni hatua ya kujivua ubinafsi na kujipa nafasi wewe na ukajitoa kwa ajili ya watu wengine.

Ni mtu pekee aliye mkomavu ambaye huona kitendo cha kujitoa si kwa ajili yake ila kwa wengine kama kitu rahisi.

Kadri unavyojitoa mwanzoni inaweza kuwa kazi, lakini muda upitavyo ndivyo kitendo hiki kinapokuwa kinaweza kuzalisha upendo na maana kubwa ya maisha ya mtu. Kujitoa kunaleta upendo mkuu na hupaisha ngazi ya juu ya utoshelevu.

Kuanguka kote katika tabia hatarishi, uraibu ni zao la usimamizi mbovu wa hisia na mawazo.




Kukosa kudhibiti mawazo na hisia ndiko kunakozalisha hatua na maamuzi mabaya yanayomuingiza mtu katika mateso na majuto.

Wajibu makini wa kusimamia fikra kwa mtu mwenyewe ni kupunguza mateso yanayoweza kuzalishwa na hatua zinazoongozwa na hisia hasi na mawazo mabaya.

Kujizuia ni mlango wa uhuru na maisha yalio salama. Wengi wameingia katika mateso makubwa sababu ya kukosa kujizuia tamaa zao.

Maisha ya mtu ambayo yanakosa kujizuia ni maisha yasiyo na kinga yanayoweza kushambuliwa na chochote kile na wakati wowote ule.

Mtu huanza kuona yupo huru pale ambapo ataweza kujitawala mwenyewe na kutawala hisia na mawazo yake mwenyewe.

Hekima ni njia kuu ya kuishi kwa furaha na ndipo ilipo furaha kuu ya maisha. Hekima ni ulinzi wa fikra na nafsi ya mtu. Hekima ni kiongozi wa kiasi na hutambua jambo jema na baya.

Hekima inapatikana katika utendaji, mbali na watu wasemavyo hupatikana kwa kusoma vitabu, kutembea au kusoma falsafa.

Utendaji wa mambo katika maisha ndiko kunamtambulisha mtu kuwa huyu ana hekima au mpumbavu.

Mwandishi anasema njia ya kuiendea hekima ni wazi japo wengi hukwepa kuiendea na hapo ndipo maisha ya mateso yanapobisha hodi kwao.

Vitu au hali kubadilika ni kazi ya asili. Hakuna kitu au hali hubakia kuwa hivyo daima. Hata fikra nazo huendelea kubadilika kutokana na hali mbalimbali mtu atakazopitia.

Watu hukua na kadri anavyopanda ngazi ya juu ndivyo anavyoona udhaifu na makosa mengi ambayo kwa wakati huo kwa kukosa maarifa ya juu alifanya kwa ujinga.

Hivyo makosa, udhaifu, mateso na maumivu ni hali ambazo huendelea kumfuatilia mtu maisha yake yote.

***Mchambuzi wa kitabu hiki ni Dk. Raymond Nusura Mgeni. Anapatikana kupitia anwani raymondpoet@yahoo.com +255 676 559 211***



## WADAU SABATO KASIKA

**BAADHI ya watu wanatafsiri visivyo sera ya utoaji elimu bure kiasi cha kusababisha wengine kujiweka pembeni katika suala zima la uboreshaji wa elimu. Wadau wana maoni gani?**



### GERALD MKUYA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

UAMUZI wa serikali kutoa elimu hauna maana kwamba mtu ambaye anaweza kuchangia chochote kwa maendeleo ya shule asifanye hiyo, hiyo tafsiri inayolenga kupotosha ukweli.

Wapo ambao wamekuwa wakiamini hivyo na kufikia kukataa hata kuchangia chakula kwa ajili ya watoto wao. Ina maana wanataka serikali itoe elimu bure na pia inunue chakula kwa mfano kwa ajili ya kambi za taaluma kwa wanafunzi? Ninauliza hivyo kwasababu zimekuwepo taarifa kutoka maeneo mbalimbali nchini zikihusu baadhi ya wazazi na walezi ambao hawataki kabisa kusikia uchangiaji wa chakula kwa ajili ya kambi za taaluma.

Hii haiingii akilini kabisa, yaani mzazi anakataa kuchangia chakula kwa ajili ya maendeleo ya mtoto wake shuleni! Siyo kambi za taaluma tu bali wazazi na walezi wanatakiwa kuchangia pia ili watoto wao wanywe uji asubuhi na hata chakula cha mchana angalau waweze kusoma wakiwa wametulia kuliko kushinda na njaa.

Ninadhani ni vyema sasa wazazi na walezi wa aina hii waelimishwe watambue wajibu wao. Serikali inagharimia mambo muhimu yaliyokuwa yanawaumiza, lakini mahitaji mengine yakiwamo ya daftari, sare, viatu na chakula, wazazi wanatakiwa kugharimia.



### SHAWEJI MKUMBULA (DIWANI WA KATA YA MAGOMENI DAR)

NINACHOAMINI ni kwamba ili kufikia mafanikio ni lazima kupitia changamoto mbalimbali na ndio maana hata kwenye sera ya elimu bure kumekuwa na mkanganyiko kati ya wadau wa elimu, wazazi na walezi wa wanafunzi kuhusu suala la namna ya kutekeleza utoaji elimu bure.

Mkanganyiko huo ambao hasa ni wa kushindwa kuelewa kile ambacho serikali imekikusudia katika utaratibu wa utoaji elimu bure, ni changamoto kwenye elimu. Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Profesa Joyce Ndalichako alishaweka wazi kwamba serikali haijakataza wazazi kwa hiari yao kuweka utaratibu wa kuchangia chakula au michango mingine kwa ajili ya maendeleo ya shule. Lakini wanajitokeza baadhi ya wazazi wanashikilia msimamo ambao kwa kweli unaweza kuathiri watoto wao kielimu.

Kama ni watu wa kufuatilia taarifa mbalimbali, waziri aliwahi kusema bungeni kuwa hakuna mahali ambapo serikali ama kwa kupitia waraka au ufafanuzi wowote ambao umetolewa na viongozi ukikataza wazazi kwa hiari yao kuweka utaratibu wa chakula na michango mingine shuleni. Binafsi sioni kama kuna tatizo kama kamati za shule na bodi zitakaa na kukubaliana kufanya jambo fulani kwa maendeleo ya shule. Hao wasiotaka wanakuwa na ajenda zao za siri na zinatakiwa kukatalIwa na kila mpenda maendeleo ya shule ili waache kuleta mkanganyiko usio wa lazima na kusababisha usumbufu.



### SAFINA SEKUBA (MWALIMU CHUO CHA UALIMU MAMIRE, MANYARA)

MOJA ya vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Tano ni utoaji wa elimu bure ili kupanua wigo na kuhakikisha watoto wote wa Kitanzania wanapata elimu. Kwa kweli uamuzi huo umeongeza wingi wa wanafunzi wanaondikishwa darasa la kwanza kila mwaka, kwasababu changamoto zote ambazo wazazi walikuwa wakikumbana nazo zikiwamo za kuombwa pesa kwa kisingizio kwamba ni kwa ajili ya kununulia madawati, zimeondolewa.

Pamoja na hayo ni lazima nikubali kwamba kila penye mafanikio pana changamoto zake. Kwa mfano kwa sasa walimu wanakumbana na changamoto inayotokana na wingi wa wanafunzi darasani. Katika mazingira hayo ufundishaji unaweza kuwa mgumu. Kwa hiyo uboreshaji wa elimu bado unahitajika, hasa katika kuongeza vyumba vya madarasa ili wanafunzi wasilundikane katika darasa moja. Vilevile kuna tatizo la ukosefu wa vitabu shuleni na matatizo mengine mengi ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu hata kabla ya utoaji wa elimu bure. Kwa hiyo jamii bado ina nafasi ya kushiriki katika uboreshaji wa elimu kwenye maeneo yao badala ya kuachia serikali tu.



### LUCAS MSIMBETE (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

HAPA kinachotakiwa ni kuendelea kuielimisha jamii kwamba ushiriki katika suala zima la elimu ni jambo la msingi na la tija. Kukua kwa jamii kunategemea kimsingi mwamko wa jamii yenyewe katika masuala mtambuka. Elimu hii ianzie ngazi ya familia, wananchi kufuatilia kwa karibu mahitaji ya shule ili kusaidiana na serikali kutatua changamoto zilizopo, hivyo kuchochea mabadiliko chanya katika elimu.

Ni muhimu kushirikiana na serikali kwenye utekelezaji wa sera zake. Kwa mfano Tanzania ya viwanda, wananchi washiriki kikamilifu katika maendeleo ya elimu ili taifa lipate wataalam wa kutosha na wenye weledi kuleta tija katika uzalishaji. Pia serikali bila shaka ina wajibu mkubwa kuhakikisha shule zinakuwa na walimu wa kutosha na wenye ujuzi unaostahili katika muktadha wa uelimishaji na pia serikali na wananchi ni muhimu kuhakikisha kuna miundombinu ya kutosha shuleni na kuweka mazingira salama ya watoto kujifunzia. Yaani mazingira yanayosaidia walimu na wanafunzi kutekeleza majukumu yao kikamilifu ili kuandaa wananchi wenye sifa zinazostahili katika ujenzi wa uchumi wa taifa.



### MARIA MTOLELA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

SERIKALI kupitia kwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Profesa Joyce Ndalichako imekuwa ikibainisha changamoto zinazokabili elimu ya msingi kuwa ni pamoja na ongezeko kubwa la uandikishaji wa wanafunzi katika elimu ya awali na msingi, ambalo serikali inazifanyia kazi ili kuweza kuzipatia ufumbuzi.

Lakini pia zipo changamoto za upungufu wa miundombinu ya madarasa, vyoo na mahitaji mengine ya kujifunzia na kufundishia na kwamba wanafunzi wengine wanatembea umbali mrefu kufuata elimu.

Mimi ninampongeza waziri kwa kusema ukweli kuhusu hali halisi ilivyo kwenye sekta ya elimu. Kinachotakiwa ni sisi wananchi kuona ni jinsi gani tunaweza kushiriki katika kumaliza changamoto hizo badala ya kuiachia serikali tu. Ni kweli imetangaza kutoa elimu bure, lakini hatuna budi kujiongeza na kuona ni wapi tunaweza kusaidia kwani hatujazuiwa.



## Sekta isiyo rasmi kushiriki Mei Mosi

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WAFANYAKAZI wa sekta isiyo rasmi nchini wanatarajiwa kushiriki kwa mara ya kwanza katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi (Mei Mosi) mwaka huu, baada ya kutambuliwa rasmi na serikali pamoja na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini (Tucta).

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Mbeya, Katibu Mtendaji wa Kamati ya taifa ya kuratibu shughuli za wajasiriamali na wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi, Constantine Lubawa, alisema kwa mara ya kwanza wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi, wamealikwa kushiriki maadhimisho hayo.

Alisema wafanyakazi wa sekta hiyo wakiwamo wajasiriamali kutoka Mkoa wa Mbeya watakaoshiriki kwenye maadhimisho hayo watawakilisha wenzao nchi nzima ambao hawataweza kufika kutokana na sababu mbalimbali.

Lubawa alisema Kamati ya kitaifa ya kuratibu shughuli za wajasiriamali na wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi, wanaishukuru serikali ya awamu ya tano chini ya Rais, Dk. John Magufuli kwa kuwatambua wajasiriamali na kuamua kuwapatia vitambulisho maalumu.

"Tunaamini kuwa sasa serikali imeonyesha kututambua, sasa tutatumia maadhimisho hayo kumuomba Rais Magufuli atusaidie wakati huu wa uongozi wake atuwekee misingi mizuri itakayotuwezesha kupata sera nzuri itakayotufanya tutambuliwe kisheria," alisema Lubawa.

Aidha, aliwataka wajasiriamali na wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi kutambua kuwa kuna kamati iliyoundwa kwa ajili ya kuratibu shughuli zao kitaifa na hivyo wanatakiwa kufanya kazi kwa kujiamini.

Aliyataja baadhi ya makundi ambayo yapo kwenye sekta isiyo rasmi kuwa ni pamoja na mama na baba ntilie, waendesha pikipiki za abiria (Bodaboda) na bajaji, wafanyakazi wa ndani na wafanyakazi wa baa.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Shughuli za Wajasiriamali na Sekta Isiyo rasmi, Ashura Seng'ondo, alisema kwa sasa wanakusudia kuzunguka katika mikoa yote nchini kuitambulisha kamati hiyo kwa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi.

Alisema chombo hicho kiliundwa mwezi Juni mwaka 2018, lakini bado hakijatambulika kwa wajasiriamali wengi na ndio maana wameamua kuanza kukitambulisha kwa wananchi.

# GGM mshindi usalama na afya mahala pa kazi

Na Nebart Msokwa, MBEYA

KAMPUNI ya uchimbaji wa madini ya dhahabu ya Geita Gold Mine (GGM) mkoani Geita, imeibuka mshindi wa jumla kwenye mashindano ya usalama na afya mahala pa kazi kwa kujizolea tuzo tatu zilizokuwa zimeandaliwa na Wakala wa Usalama na Afya mahala pa kazi nchini (Osha).

Kampuni hiyo ilinyakua tuzo hiyo juzi wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya mahala pa kazi duniani ambayo kitaifa yalifanyika jijini Mbeya na kushirikisha washiriki 40 kutoka mikoa yote nchini.

Akiwakabidhi tuzo hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uratibu wa Bunge, Sera, Kazi, Ajira na watu wenye ulemavu, Jenista Mhagama, aliipongeza kampuni hiyo kwa kuzingatia sheria na taratibu za usalama na afya mahali pa kazi.

Alizitaka kampuni mengine kuzingatia sheria hiyo ili kuwalinda wafanyakazi wao na kuongeza tija ya uzalishaji kwenye maeneo yao kwa madai kuwa endapo hawatazingatia sheria hiyo wanaweza wakapelekea wafanyakazi wao kupata madhara.

**Mwaka jana maonyesho hayo yalifanyika mkoani Iringa na kushirikisha kampuni 18 pekee, lakini mwaka huu yameshirikisha kampuni 40 kutoka mikoa mbalimbali nchini.**

"Nawaagiza waajiri wote nchini kuzingatia matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya mahali pa kazi ili kuwalinda watumishi wao na kuwawezesha wao na familia zao kuendesha vizuri za maisha yao, nawapongeza sana GGM wamekuwa wakifanya vizuri sana," alisema Mhagama.

Ofisa Mawasiliano wa GGM, Theophil Pima, alisema mbali na kuibuka na ushindi, pia kupitia maonyesho hayo wamepata fursa ya kujifunza mbinu zingine kutoka kwenye kampuni zingine zilizokuwapo kwenye maonyesho hayo.

Alisema kuibuka na ushindi kwenye maonyesho hayo kumetokana na kuzingatia sheria na kanuni za usalama na afya mahali pa kazi kwa wafanyakazi wote wakati wa utekelezaji wa majukumu ya kampuni hiyo.

"Serikali imekuwa ikitoa maelekezo kila mwaka na hata maofisa kutoka Osha huwa wanatembelea maeneo yetu na kutuhamasisha kuzingatia sheria, hivyo sisi kama kampuni tuna vifaa mbalimbali vya kuwakinga wafanyakazi dhidi ya madhara yote yanayoweza kuwapata," alisema Pima.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko, aliitaka migodi yote nchini na taasisi zilizo chini ya wizara yake kufanya kazi kwa kuzingatia sheria ya usalama na afya mahali pa kazi ili kuwalinda wafanyakazi wao.

Alisema endapo wamiliki hao watazingatia vizuri sheria hiyo pamoja na kanuni zake watasaidia pia kulinda jamii ya Watanzania wanaozunguka maeneo ya migodi hiyo.

Awali akitoa taarifa ya maadhimisho hayo, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Osha, Khadija Mwenda, alisema maadhimisho ya mwaka huu yamekuwa na washiriki wengi kuliko ilivyokuwa mwaka jana.

Alisema mwaka jana maonyesho hayo yalifanyika mkoani Iringa na kushirikisha kampuni 18 pekee, lakini mwaka huu yameshirikisha kampuni 40 kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Alisisitiza kuwa Tanzania kwa sasa ni miongoni mwa mataifa duniani ambayo yanatekeleza kwa vitendo Sheria ya Usalama na Afya mahali pa kazi kwa maelezo kuwa matukio ya ajali kazini yamepungua sana.

"Lakini pamoja na kwamba tunaonekana kuwa tuko vizuri, lakini tukumbuke kuwa tunaelekea kwenye uchumi wa kati ambao unaendana na maendeleo ya viwanda, kuna hatari ya kuongezeka kwa matukio ya ajali hivyo lazima tuendelee kutoa elimu," alisema Mwenda.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, akifuatilia takwimu za ajali zitokanazo na shughuli za uchimbaji katika Mgodi wa Dhahabu wa Bulyanhulu, alipotembelea banda la mgodi huo kujionea namna wanavyofanya kazi wakati wa maadhimisho ya Usalama na Afya Mahali Pa Kazi Mkoani Mbeya juzi. **PICHA: OWM**

# Wakazi wapata matumaini ya maji ya bomba

Na Nebart Msokwa, MBEYA

BAADHI ya wakazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamesema wameanza kupata matumaini ya kuanza kupata maji ya bomba baada ya Rais Dk. John Magufuli kutoa maagizo kwa viongozi akiwamo Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa.

Wananchi hao walisema wamekuwa wakiahidiwa kwa muda mrefu bila utekelezaji wa aina yoyote hali iliyowafanya wakate tamaa, lakini agizo la rais limefufua matumaini yao.

Mmoja wa wananchi hao, Sarafina Mwakifuna, alisema changamoto hiyo ya uhaba wa maji imekuwa ikiwatesa zaidi wanawake na watoto ambao ndio huwa wanahangaika kwenda kutafuta huduma hiyo.

Alisema baada ya serikali kuamua kuiunganisha Mamlaka ya Maji ya Miji wa Mbalizi na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya- WSSA), walianza kupata maji kwa mgawo ambao bado ulikuwa ni wa mateso.

"Wengi hatuna mabomba ya maji majumbani mwetu kwahiyo huwa tunachota kwenye vituo vya jumuiya, wakati mwingine unakuta mgawo wa eneo letu ni usiku sana hivyo huwa tunahatarisha maisha kwa kuamka kwenda kuchota," alisema Sarafina.

Naye Sabrina Chale, alisema kutokana na shida ya maji inayowakabili wakazi wa mji huo, wanalazimika kununua kwa dumu moja la lita 20 kwa Sh. 500 kutoka kwa vijana ambao huwa wanatembeza kwenye matolori. Alisema wakati mwingine maji hayo huwa usalama wake sio wa uhakika kutokana na vijana hao kuchota hata kwenye visima na vijito vidogo ambavyo si salama.

Alisema endapo wataanza kupata maji mwishoni mwa mwezi Mei ama Juni kama alivyoagiza rais, watakuwa wamekombolewa.

Alipokuwa anaanza ziara yake mkoani Mbeya Aprili 25, mwaka huu, Rais Dk. John Magufuli, alimpa mwezi mmoja Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Makame Mbarawa, kuhakikisha anakamilisha mradi wa maji unaogharimu zaidi ya Sh. bilioni tatu.



# Watakiwa kuitunza miradi ya wadau wa maendeleo

**Na Ibrahim Joseph,** CHEMBA

WANANCHI wametakiwa kuhakikisha wanaitunza na kuendeleza miradi ya maendeleo inayokabidhiwa katika maeneo yao na wadau wa maendeleo.

Rai hiyo ilitolewa na Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Deogratius Ndejembi, wakati alipokuwa akipokea mradi wa maendeleo ya jamii Sanzawa AP kutoka Shirika la World Vision Tanzania.

Ndejembi aliwataka wananchi kuhakikisha wanatunza na kuendeleza miradi ya maendeleo inayokabidhiwa na wadau wa maendeleo kwenye maeneo yao.

"Wafadhili wanapotuletea miradi ya maendeleo, mjue ipo siku watamaliza muda wao, hivyo ni jukumu letu wananchi kuhakikisha mnaitunza na kuendeleza miradi hiyo inayoletwa kwetu," alisema.

**Kuna baadhi ya watu wamekuwa wakihodhi miradi ya maji inayoanzishwa katika maeneo yenu na kuwakosesha wananchi huduma, nawaonya nikiisikia hiyo nitawawajibisha wote bila kumwogopa mtu.**

Alisema miradi hiyo ni mali ya wananchi, hivyo wafadhili wanapomaliza muda wa kutekeleza inakabidhiwa kwao, wakumbuke kuiendeleza ili kutowakatisha tamaa kuendelea kutoa huduma kwenye maeneo mengine.

Kuhusu miradi ya maji, aliwataka viongozi wa vijiji na wananchi kuhakikisha wanashirikiana katika kusimamia vizuri ili kuwanufaisha watu wote.

"Kuna baadhi ya watu wamekuwa wakihodhi miradi ya maji inayoanzishwa katika maeneo yenu na kuwakosesha wananchi huduma, nawaonya nikiisikia hiyo nitawawajibisha wote bila kumwogopa mtu," alisema.

Akisoma risala ya wanajamii wa kijiji cha Sanzawa, Fatuma Ally, alisema mradi huo umewanufaisha watu takribani 27,395 katika maneo mbalimbali.

Alilishukuru Shirika hilo kupitia wafadhili wa Ireland kwa namna walivyojitoa kwa hali na mali ili kuhakikisha wanasaidia wananchi wa maeneo yenye changamoto tangu mwaka 1999.

Aidha, alisema mradi uliwasaidia wakulima kupata elimu ya kilimo bora na kuanzishwa kwa vikundi vya kuweka na kukopa.

Aliongeza kuwa mradi huo ulifanikiwa kuwajengea madarasa 70, nyumba 41 za walimu, na madawati 1,133 yalitolewa na shirika kwa kushirikiana na jamii.

Kaimu Mkurungenzi Mkuu wa Shirika la World Vision Tanzania, Joan Kiiza, alisema shirika hilo lilianza kazi katika eneo hilo tangu mwaka 1999 na mradi huo umefikia mwisho mwaka huu.

Alitaja thamani ya miradi iliyotekelezwa katika mradi wa Sanzawa ni zaidi ya Sh. bilioni 10 zilizotumika katika kutekeleza miradi mbalimbali.

Kiiza alisema shirika hilo kupitia mpango wa 2016/2020 linatekeleza miradi yenye kipaumbele katika sekta mbalimbali ikiwamo uwezeshaji kiuchumi, afya, lishe, maji na utetezi wa haki za watoto.




Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Atashasta Nditiye (kushoto), akipatiwa maelezo ya shughuli za mawasiliano za kampuni ya Zantel kutoka kwa Meneja Mawasiliano wa kampuni hiyo, Rukia Mtingwa, alipotembelea banda la maonyesho la kampuni hiyo katika maonyesho ya maadhimisho ya miaka 10 ya UCSAF, jijini Dodoma jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Shirika lasaidia damu chupa 100

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHIRIKA la Compassion International Tanzania, limejitolea kuchangia damu chupa 100 ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya kutimiza miaka 20 tangu kuanzishwa kwake likiwa na lengo la kuhudumia watoto.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa wakati wa utoaji damu katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, Meneja wa Shirika hilo Kanda ya Kati, Ratifa Sekajiongo, alisema maadhimisho hayo ni pamoja na utoaji wa damu pia utaambatana na upandaji miti.

